Ijumaa Desemba 1, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581601

nipasheTZ nipasheTZ
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com



ARTETA: NI ZAIDI YA NDOTO ZANGU

UKURASA 22

UKURASA WA 2

**BAKWATA** yaunda msimamizi elimu Kiislamu shuleni




UKURASA WA 4

**Serikali** yafanya utafiti kilichoko nyuma ya pazia wanaoacha shule



UKURASA WA 4

**Familia** ya askofu yalishtaki kanisa kuipoka kiwanja



SIKU YA UKIMWI

# Aliyetibu mgonjwa wa kwanza alonga

• **Ana** miaka 93; asimulia mtihani wake, alivyotekeleza majukumu kwa hofu... *Endelea ukurasa 12*



Msekwa



Mwakawago



Kawawa



Gama



Mangula



Makamba



Mukama



Kinana



DK. Bashiru



Daniel Chongolo

# Kila mmoja na yake; makatibu wakuu CCM 1977 hadi Chongolo

UKURASA 2

**"Dk. Lawrence Gama aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora wakati huo, aliteuliwa kushika nafasi hiyo hadi mwaka 1997 alipomwachia kijiti Philip Mangula aliyeshika nafasi hiyo hadi Julai, 2006.**

MICHEZO **JWANENG MIKONONI MWA BENCHIKHA** UK.24

KATUNI UK.6



Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akiwa ameambatana na baadhi ya Maofisa wa Jeshi la Israel katika Kijiji cha Kfar Aza Kibbutz nchini Israel mapema wiki hii, ambacho ni kati ya vijiji vilivyoshambuliwa na wanamgambo wa Hamas Oktoba 7, 2023 ili kujionea hali halisi ya mashambulizi ilivyokuwa. Habari Uk. 7. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Kila mmoja na yake; makatibu wakuu CCM 1977 hadi Chongolo

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) ndicho chama kikongwe nchini. Ifikapo Februari 5, mwakani, kitakuwa kinatimiza miaka 47 tangu kilipoanzishwa mwaka 1977.

Kuzaliwa kwake kulitokana na kuunganishwa kwa vilivyokuwa vyama vya kupigania uhuru wa Tanganyika na Zanzibar - Tanganyika African National Union (TANU) na Afro Shiraz Party (ASP).

Tangu kuanzishwa, CCM imepita katika vipindi tofauti ikiwamo kukubali kuruhusu mfumo wa vyama vingi ili kuendana na wimbi la mabadiliko ya kiuchumi na kisiasa duniani yaliyoanzia mwishoni mwa miaka ya 1980. Kutokana na mabadiliko hayo, CCM kama vilivyo vyama vipya vilivyoanzishwa, ilisajiliwa rasmi katika daftari la Msajili wa Vyama vya Siasa Julai, mwaka 1992.

CCM kupitia Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) iliafiki kuanzishwa kwa mfumo huo kama alivyoshauri Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, kuwa Tanzania si kisiwa, hivyo haina budi kuendana na mabadiliko hayo ikiwamo kuingia katika mfumo wa vyama vingi.

Kabla, CCM ilikuwa mhimili wa mageuzi na miongozo ndani ya serikali. Kama ilivyokuwa TANU mwaka 1971, mwaka 1981 ilitoa mwongozo wa uendeshaji wa nchi chini ya Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Pia mwaka 1997, ilitengeneza mpango wa miaka 15 wa kipindi cha mpito kuelekeza uchumi wa kisasa.

**MABADILIKO YA UONGOZI**

Tangu kuanzishwa na waasisi wake, CCM imepitia mabadiliko mbalimbali ya uongozi katika nafasi mbalimbali ambayo yaliendana pia na mabadiliko ya muundo ndani ya chama. Mwaka 1977 hadi 1985, Rais alikuwa ndiye mwenyekiti wa chama lakini kuanzia mwaka 1985, Nyerere aliendelea kuwa mwenyekiti licha ya kung'atuka urais.

Utaratibu huo ulirejeshwa mwaka 1990 kwa Rais pia kuwa mwenyekiti wa chama. Rashidi Mfaume Kawawa, aliyekuwa Katibu Mkuu wa CCM, alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti.

Aidha, utaratibu mwingine ulikuwa kwamba iwapo Rais atatoka upande mmoja wa Muungano, Makamu wa Rais ambaye atatoka upande mwingine, atakuwa Makamu Mwenyekiti. Pamoja na Mwinyi kuwa Rais, aliendelea kuwa makamu Mwenyekiti, nafasi ambayo aliishika kuanzia mwaka 1984 baada ya Aboud Jumbe kujiuzulu urais wa Zanzibar.

Mwaka 1997, mabadiliko zaidi yalifanyika kwa kuwa na makamu wenyeviti kutoka Zanzibar na Tanzania Bara. Aliyekuwa Rais wa awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, alichaguliwa Mwenyekiti na Dk. Salmin Amour, aliyekuwa Rais wa Zanzibar, akawa Makamu Mwenyekiti Zanzibar na John Malecela Tanzania Bara.

Mfumo huo wa uongozi tangu wakati huo uliendelea hadi sasa. Kwa sasa Rais Samia Suluhu Hassan ndiye mwenyekiti huku makamu wawili wake wakiwa Kanali Mstaafu Abdulrahman Kinana (Bara) na Dk. Hussein Mwinyi ambaye ni Rais wa Zanzibar kwa upande wa visiwani.

**MAKATIBU WAKUU**

Katika nafasi hiyo ambayo ni ya kiutendaji, kumekuwa na mabadiliko mbalimbali tangu mwaka 1977. Wakati CCM ikianzishwa, ilirithi mfumo wa TANU wa kuwa na Katibu Mtendaji Mkuu. Walioshika nafasi hiyo ni Pius Msekwa (1977 hadi 1980) na Daudi Mwakawago (1980 - 1982).

Mwaka 1982 kulifanyika mabadiliko na kuanzishwa kwa nafasi ya Katibu Mkuu huku Kawawa akishika kwa mara ya kwanza mpaka mwaka 1990 alipochaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti hadi mwaka 1997.

Horace Kolimba aliteuliwa mwaka 1990 kuchukua nafasi ya Kawawa na alidumu kwenye wadhifa huo hadi mwaka 1994. Kolimba aliondolewa kwa shinikizo kutokana na madai kwamba akiwa Katibu Mkuu alishindwa kudhibiti wimbi la wabunge 55, maarufu kama G55 waliokuwa wakitaka kuundwa kwa serikali ya Tanganyika kutokana na hoja mbalimbali.

Dk. Lawrence Gama aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora wakati huo, aliteuliwa kushika nafasi hiyo hadi mwaka 1997 alipomwachia kijiti Philip Mangula aliyeshika nafasi hiyo hadi Julai, 2006.

Yussuf Makamba alimrithi Mangula na kushika nafsi hiyo hadi mwaka 2011. Mukama alichukua nafasi hiyo, mabadiliko yaliyotokea kwa kile kilidaiwa kujivua gamba ndani ya chama kutokana na kukithiri kwa ufisadi ndani ya CCM na serikali. Hata hivyo, Mukama hakudumu sana kwa kuwa aliwekwa kando katika Mkutano Mkuu wa mwaka 2022 na nafasi yake kuchukuliwa na Kinana.

Mwaka 2018, Dk. Bashiru Ally aliteuliwa kuchukua wadhifa huo na kudumu nao hadi mwaka 2021 alipoteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Baadaye nafasi hiyo ilishikwa na Daniel Chongolo aliyeandika barua ya kujiuzulu na hatimaye Mwenyekiti Rais Samia na NEC kumkubalia.

**KAA LA MOTO**

Kwa ujumla, nafasi ya Katibu Mkuu imeonekana kuwa kaa la moto kutokana na namna baadhi ya wateule katika nafasi hiyo wanavyoingia na kutoka. Wako walioondoka kutokana na mabadiliko ya kimfumo na wengine kutokana na tofauti za kisiasa na watu wanaoingia kwenye uongozi wa nchi.

Julai 3, 2006 kwa mfano, baada ya Kikwete kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa CCM katika Ukumbi wa Chimwaga, aliitisha kikao cha NEC ndani ya muda mfupi katika ukumbi wa White House na kuiondoa sekretarieti yote iliyokuwa chini ya Mangula.

Aidha, kutokana na tuhuma zinazokikabili chama na serikali, kama ilivyokuwa mwanzoni mwa miaka ya 2010, NEC iliamua kuiondoa sekretarieti iliyokuwa chini ya Makamba kwa ajili ya kujivua gamba.

# BAKWATA yaunda chombo elimu ya Kiislamu shuleni

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amezindua chombo kinachosimamia elimu ya dini ya Kiislamu (TISTA) kikipewa jukumu la kutoa mwongozo wa kufundisha kwa wanafunzi wa sekondari.

Jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa chombo hicho, Prof. Mkenda alisema wamekamilisha maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo na kazi hiyo ilikuwa shirikishi.

"Bahati nzuri sera imepita na mitaala ni kazi ya kiufundi. Kwa kawaida hata huko nyuma mitaala huwa haiendi kwenye mabaraza ya mawaziri, inafanywa kiufundi na kupitishwa na kwenda kutumika kwenye shule," alisema.

Waziri huyo alisema kuwa mwaka huu wamefanya kazi hiyo kuwa shirikishi zaidi kwa kuwa mitaala hiyo inaakisi mfumo mpya wa elimu ambao ni tofauti kwa namna kubwa.

Alitolea mfano shule ya msingi kwa sasa ni miaka sita, lakini ni lazima mtoto kukaa shuleni miaka 10, akifafanua "ni suala la kisera, huwezi kuandaa mtaala ambao hauangalii sera".

Alisema katika mitaala hiyo, kuna masuala ya dini ambayo ina imani zake. Kukiwa na mambo hayako vizuri, busara ni kurudi na kusikiliza.

"Mitaala ya dini ni ya kipekee, haifanani na somo la Kemia. Dini inavuta hisia na ikitokea tafsiri ambayo si sahihi, tunaweza kuwa na hisia kali dhidi yake. Tuliliona hilo wakati wa kuandaa mitaala," alisema.

Prof. Mkenda alisema waliona kuna hali ya shaka kwenye mambo ya dini, hivyo kuamua kukaa kwa pamoja kuwasikiliza.

Alisema baada ya mazungumzo, walikubaliana na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Mufti Aboubakar Zuber, na kukubali ili pasiwapo shaka hiyo.

Mufti Zuber aliishukuru serikali kwa uamuzi sahihi na kuomba kufanyiwa kazi mapendekezo waliyoyatoa ikiwamo kugharamia TISTA.

Katibu Mkuu wa BAKWATA, Alhaj Nuhu Mruma, alisema uandaaji wa mapendekezo hayo umeshirikisha pande zote mbili za Muungano; Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. "Hatuna shaka kuwa serikali itatekeleza maoni na mapendekezo hayo ya 'wana dini' na kuepuka malengo mengine yasiyo mema," alisema na kusisitiza elimu ya dini ya Kiislamu ni mali ya Waislamu wenyewe.

## HABARI KITAIFA

# Mkemia mkuu abainisha muda wa upimaji sampuli dawa za kulevya

**Na Zanura Mollel**

MKEMIA Mkuu wa Serikali (CGC), Dk. Fidelice Mafimiko, amesema upimaji wa sampuli za dawa ya kulevya huchukua siku 6.5 za kazi kuchakata na kuchunguza ili mamlaka zingine zichukue hatua pindi taratibu zinapokamilika.

Dk. Mafimiko alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam juu ya kazi za Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA).

Alisema mamlaka hiyo imetekeleza majukumu ya upimaji wa sampuli kwa wakati kutokana na upatikanaji wa vitendea kazi ukiwamo mtambo maalumu (LC-MSMS) wenye thamani ya Sh. bilioni 2.9 unaotumika kupima na kuchunguza kwa haraka sumu, chanjo na viambata vilivyomo kwenye dawa na dawa za kulevya.

"Kwa sasa hakuna ubabaishaji. Majibu yanatoka sahihi na tunashiriki katika kutoa ushahidi mahakamani kwa kile tulichokibaini. Vifaa na mitambo ya kisasa vimerahisisha kazi," alisema Dk. Mafimiko.

Aidha, Dk. Mafimiko alisema mamlaka hiyo imefanya kazi kwa kushirikiana na madaktari bingwa wa binadamu kubaini jinsi za watoto wanaozaliwa wakiwa na changamoto ya utambuzi wa maumbile.

"Tunachukua sampuli na kuchunguza tunabaini jinsi na kushauriana na madaktari ili kuendelea na taratibu zingine," alisisitiza.

Alisema utaratibu wa upimaji wa vinasaba (DNA) kwa mtu mmoja ni Sh. 100,000, hivyo kwa mama, baba na mtoto ni Sh.300,000 na malipo hufanyika kwa mfumo wa malipo ya serikali (control number). Alisema gharama hizo zipo tangu mwaka 2005.

"Lengo ni kupunguza migogoro kwenye familia katika utoaji wa haki na malezi ya mtoto. Majibu yanatolewa kwa uwazi na hakuna udanganyifu. Ukitaka kufanya vipimo nenda ofisi ya ustawi wa jamii au kwa wakili wa serikali watakaandika barua ya kuomba vipimo vya DNA.

Kwa wale ambao kesi zao ziko chini ya Jeshi la Polisi, jeshi hilo litaomba kwa niaba, utakuja kufanya vipimo ukiwa umeambatana na aliyekuombea. Taratibu zingine utaelekezwa," alisema. Kuhusu utoaji wa figo, alisema wamekuwa wakizingatia uchunguzi wa DNA kwa ndugu anayetaka kumtolea mgonjwa.

"Tunajiridhisha kama vinasaba vinashabihiana ndipo tunashauriana na madaktari katika utekelezaji wa jambo hilo," alisema.

Mkurugenzi wa Huduma za Sayansi Jinai, David Elias, alisema Mamlaka ya Kuzuia na Kudhibiti Dawa za Kulevya (DCEA) ni wadau wakubwa wa GCLA,wanaohusika kudhibiti uingizwaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini. "Sisi tunapokea sampuli kupima dawa za mimea ya asili mfano bangi na mirungi, dawa za asili zilizochanganywa na kemikali ili kupata heroin na ccaine pamoja na dawa zinazotengenezwa kwa kutumia kemikali bashirifu mfumo wa vidonge.

"Kesi zinazoongoza kupokelewa katika upimaji ni mashauri ya jinai zikiwamo kesi za dawa za kulevya huku jinai ikihusisha mauaji, ubakaji, ulawiti na ujangili wa wanyamapori," alisema.

# Askari wanyamapori 6 kortini tuhuma mauaji

**Na Halima Ikunji,** TABORA

ASKARI sita wa kikosi cha Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori Tanzania (TAWA), wamepandishwa kizimbani Mahakama Kuu ya Kanda ya Tabora kwa tuhuma za mauaji ya watu sita kwa kuwachoma moto na baiskeli zao katika hifadhi ya Ugalla.

Waliopandishwa kizimbani ni Shoka Haruna, David Laurence, Mussa Nyarukende, Rosta Muhigi, Ally Musa na Abasi Rajabu kwa tuhuma za mauaji ya kukusudia.

Kesi hiyo iko mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora, Zainabu Mango na mashahidi 26 akiwamo Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Tabora Mrakibu wa Polisi, Kisu Andondile.

Akitoa ushahidi wake jana Andondile alidai kupokea taarifa ya watu sita kuuawa kwa kuchomwa moto katika tukio lililotokea Julai 27, mwaka 2022.

Alidai baada ya kusikia taarifa hiyo alimweleza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Richard Abwao na baadaye walielekea eneo la tukio na kukuta baiskeli 12 zikiwa zimechomwa moto, vipande vya mbao, maganda manne ya risasi ambazo zinatumika kwenye silaha aina ya SMG.

Alidai baada ya kukuta hali hiyo, walianza kuitafuta miili ya watu hao, lakini kwa siku hiyo hawakuiona ikidaiwa kuwa ilihamishwa na kupelekwa eneo lingine.

Alidai baada ya kuhojiwa watuhumiwa hao walikiri kufanya tukio hilo na waliwapeleka eneo ambalo baada ya kuwafanyia mauaji walikwenda kuwatupa umbali wa mita 87 kutoka hifadhini.

Baada ya kufanya upelelezi huo walibaini kuwa washtakiwa hao walikuwa katika doria siku hiyo ikilinganisha maganda ya risasi za silaha ya SMG ambayo walikuwa nayo.

Mkuu huyo wa upelelezi alidai walipokwenda katika eneo hilo waliikuta miili mitano na mmoja kuonekana kuliwa na mnyama, na haikuweza kutambulika na ndugu kutokana na kuchomwa moto.

Alidai baada ya miili hiyo kutokutambulika, ulifanyika uchunguzi wa kitabibu kwa kuchukua vipimo kwa kuunganisha vinasaba kwa ndugu wa marehemu ili kuwatambua ndugu zao na kuruhusu waende kufanya maandalizi ya mazishi.

Baada ya ushahidi wa Andondile, Jaji Mango aliahirisha kesi hiyo na itaendelea kusikilizwa leo kwa kuendelea kupokea ushahidi kutoka upande wa Jamhuri.

Upande wa Jamhuri inasimamiwa na Wakili Stivin Mzava, Merito Ukongoji, Alis Thomasi na Nurdin Mmari huku upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili Kelvin Kayaga na Akram Magoti.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Telegram: "Uvuvi"
Simu: 255 026 2322612
Fax: 255 026 2322613
E-Mail: ps@uvuvi.go.tz
Web:http://www.mifugouvuvi.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Ulinzi,
S.L.P 2847,
40487 DODOMA.

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUFUNGULIWA KWA UVUVI WA KAMBAMITI KWA MSIMU WA MWAKA 2024**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi inapenda kuwatangazia wananchi wote kuwa uvuvi wa Kambamiti (Prawn Fishery) kwa msimu wa mwaka 2024 utafunguliwa tarehe 1 Machi, 2024 na utafanyika hadi tarehe 30 Septemba, 2024 kwa Kanda ya Kaskazini inayohusisha maeneo ya Dar Es Salaam, Tanga, Bagamoyo na Saadani na tarehe 01 Aprili 2024 hadi tarehe 31 Agosti, 2024 kwa Kanda ya Kusini inayohusisha maeneo ya Kisiju, Rufiji delta, Jaja/Kilwa, Lindi na Mtwara.

Kwa tangazo hili, kila Kampuni au mwananchi mwenye nia ya kufanya uvuvi wa Kambamiti kwa msimu wa mwaka 2024 anaombwa kutuma maombi kuanzia tarehe 01 Disemba, hadi tarehe 15 Disemba, 2023. Waombaji wanapaswa kuzingatia Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003, Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009 na Marekebisho yake ya Mwaka 2020. Pia, vigezo vya kuzingatia katika maombi ya uvuvi tajwa vinapatikana katika Tovuti ya Wizara **(www.mifugouvuvi.go.tz)** na katika Ofisi za Wizara Kanda ya Dar Es Salaam na Pwani.

Maombi ya leseni za uvuvi wa Kambamiti kwa wavuvi wadogo yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika na wavuvi wakubwa maombi yatumwe kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Imetolewa na:

**Prof. Riziki S. Shemdoe**
**KATIBU MKUU**



SHANGHAI MITSUBISHI ELEVATOR
S.E.C
COMPLETE LIFT SOLUTION FOR BUILDINGS

**TANGAZO KWA UMMA**




Mr.Emilian C.Kimaro
Mr.Nelson J.Gilson

Wenye majina tajwa na picha zao hawafanyi kazi tena na S.E.C. (East African) Company Limited tangu 2022. Kampuni haitawajibika kwa majukumu yao yoyote au shughuli zozote .ambazo watafanya kwa niaba ya kampuni




S.E.C. (EAST AFRICAN) CO. LTD
P.O. Box 8454, Tanesco Street, Msasani, Dar es Salaam, Tanzania
sales@mitsuelevator.com / md@mitsuelevator.com
+255 713-324415 / +255 713-335758
www.mitsuelevator.com




Mkurugenzi Mkazi wa Amref Health Africa Tanzania, Dk. Florence Temu (katikati), akitoa maelezo kwa Mratibu wa Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kukabiliana na UKIMWI (PEPFAR) nchini Tanzania, Jessica Greene (wa pili kushoto) na Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Kimarekani la Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa (CDC), Dk. Mahesh Swaminathan (wa tatu kulia), walipotembelea banda la Amref Tanzania wakati wa maonyesho ya shughuli zinazofanywa na wadau katika mapambano dhidi ya UKIMWI katika viwanja vya Morogoro Sekondari mkoani Morogoro jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Familia ya askofu yalishtaki kanisa

## -Ni madai ya kupoka ardhi, kumpa mwekezaji

**Na Grace Gurisha**

FAMILIA ya marehemu Askofu Mkuu John Sepeku wa Kanisa Anglikana Tanzania Dayosisi ya Dar es Salaam, imefungua shauri katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kitengo cha Ardhi kupinga kunyang'anywa zawadi ya kiwanja alichopewa marehemu baba yao na waumini wa dayosisi hiyo mwaka 1978.

Shauri hilo namba 378/2023 limefunguliwa na mtoto wa marehemu, Bernardo Sepeku dhidi ya Bodi ya Wadhamini Kanisa Anglikana Tanzania, Askofu Jackson Jackson Dayosisi ya Dar es Salaam Anglikana na Kampuni ya Xinrong Plastic Waste Industry Co Ltd.

Bernardo ambaye ni msimamizi wa mirathi ya baba yake, anaiomba mahakama iamuru kanisa hilo kuzingatia azimio lao lililopitishwa na taasisi yao ili kumwezesha kuandika na kuorodhesha ya mali za baba yake, Askofu Sepeku.

Bernardo pia anaiomba mahakama hiyo imwamuru mshtakiwa wa kwanza, wa pili na wa tatu kwa pamoja kulipa Sh. milioni 33 ikiwa ni hasara aliyoipata mlalamikaji kutokana na uharibifu wa mazao yaliyowekezwa katika shamba lililomo ndani ya kiwanja namba 2689 huko Buza, Temeke.

Baadhi ya mazao yaliyoharibiwa shambani ni miti ya michungwa, minazi, mihogo, miti ya mipapai, miti ya malimao na miembe.

Mlalamikaji huyo pia anataka alipwe Sh . bilioni 3.72 ikiwa ni fidia ya hasara ya kifedha iliyopatikana kutokana na uvamizi wa mali ya ardhi iliyoko katika kiwanja hicho na wanaomba fidia ya Sh. milioni 493.65 ikiwa ni faida iliyotarajiwa ambayo ingepatikana baada ya kukomaa na mavuno ya mazao yaliyokuwamo kwenye shamba hilo.

"Waumini/wakristo wa dayosisi ya Dar es Salaam walimpa zawadi kwa kazi nzuri na upendo waliokuwa nao kwa Askofu Sepeku mwaka 1978 na baadaye kuidhinishwa na Mkutano Mtakatifu wa Sinodi ya Dayosisi ya Dar es Salaam Kanisa la Anglikana katika kikao chake cha sinodi kilichofanyika mwaka 1980, kiliamua kutoa zawadi," alidai Bernardo.

Inadaiwa Kanisa la Anglikana Tanzania kwa kushirikiana na Askofu wa Dayosisi ya Dar es Salaam limechukua kiwanja hicho na kumpatia mwekezaji kutoka China.

Shauri hilo namba 378/2023 linatarajiwa kutajwa tena katika mahakama hiyo Februari 12 mwaka huu mbele ya Jaji Arafa Msafiri.

# Tanzania mwenyeji mkutano wa kimataifa usonji, mtindio ubongo

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA inatarajiwa kuwa mwenyeji wa mkutano wa kimataifa unaolenga kujadili changamoto zinazohusiana na usonji na mtindio wa ubongo utakaofanyika kwa siku mbili kuanzia kesho katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.

Mkutano huo umeandaliwa kwa ushirikiano baina ya taasisi ya Victorious Centre of Excellence na Autism Connect. Victorious Centre of Excellence ni kituo kinachotoa huduma mbalimbali za tiba ya urekebishaji na shughuli za ziada kwa watoto wenye hali ya usonji nchini kwa lengo la kuwajumuisha katika jamii kupitia mikakati ya kujenga uelewa wa kijamii.

Autism Connect ni taasisi ya kimataifa iliyojikita kwenye kueneza ufahamu, kutoa elimu na kuwezesha utunzaji wa kina kwa watu wenye changamoto za usonji kwa nchi mbalimbali duniani.

Juhudi hizo za pamoja zimefanikisha kuandaliwa mkutano huo wa siku mbili ambao utakuwa na lengo la kuongeza ufahamu kuhusu usonji na kutoa jukwaa kwa wataalamu kutoka duniani kote kubadilishana uzoefu na kujadili maendeleo ya hivi karibuni kuhusiana na changamoto hiyo.

Mgeni rasmi kwenye mkutano huo anatarajiwa kuwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya. Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa taasisi ya Victorious Centre of Excellence ambaye pia ni Mwenyekiti wa Mkutano huo, Sarah Laiser alieleza kufurahishwa kwake na mkutano huo, akisema:

"Tunafuraha kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huu muhimu, kwani unatoa fursa maalum kwa wataalamu wa matibabu kuungana na wenzao kutoka maeneo mbalimbali duniani wanaoshughulika na changamoto ya usonji."

Alisema mkutano huo unalenga kuwezesha kubadilishana mawazo na matokeo ya kimatibabu kati ya wazazi na wataalamu na hatimaye kupelekea huduma bora kwa watu binafsi walio na changamoto hiyo.

Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wa mkutano huo kutokana na changamoto za kipekee ambazo Bara la Afrika zinalikumba katika kukabiliana na usonji, kwa mujibu wa waandaaji hao.

"Kuongezeka kwa watu wenye changamoto ya usonji ni jambo linalotia wasiwasi mkubwa. Kituo cha Kudhibiti Magonjwa (CDC) cha Marekani kinaripoti takwimu za kustaajabisha.

"Katika kila watoto 36, mmoja nchini Marekani amegundulika kuwa na changamoto ya usonji. Utafiti unafafanua kwamba kati ya watoto 37 wa kiume, mmoja wao huwa na changamoto ya usonji.

"Zaidi, utafiti umebaini kati ya watoto 157 wa kike, mmoja wao hubainika na changamoto ya usonji. Hii inaonesha watoto wa kiume hupatwa na tatizo hili mara nne zaidi ya watoto wa kike," alisema.

Alibainisha kuwa kwa Tanzania, takwimu zinaonesha ongezeko kubwa la tatizo hili katika miongo miwili iliyopita, hivyo kuhitajika kuchukua hatua madhubuti.

Alisema watoto walioathiriwa na usonji hukumbana na changamoto katika mawasiliano, kushindwa kutamka maneno vizuri, hukabiliwa na ugumu katika kupokea mafunzo ya kielimu na mara nyingi huonyesha tabia za ukorofi kupindukia.

Akizungumzia mkutano huo, Dolly Thakkar, Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa taasisi ya Autism Connect, alisema mkutano huo utawaleta pamoja wataalamu kutoka Tanzania, Kenya na Uganda pamoja na wajumbe kutoka sehemu mbalimbali za dunia. Alisema mkutano huo utashirikisha wazungumzaji mashuhuri kutoka nchi mbalimbali duniani zikiwamo mwenyeji Tanzania, Uingereza, Zimbabwe, Kenya, India, Marekani, Afrika Kusini, Ubelgiji, Italia na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

"Jambo zuri ni kwamba Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, atapamba mkutano huo kwa kuwapo kwake. Mahudhurio yake yanaashiria wazi dhamira na msaada wa serikali katika kuboresha maisha ya watu wenye usonji nchini," alisema.

# Serikali yafanya utafiti kubaini kilichojificha wanaoacha shule

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema hawajaridhishwa na takwimu za waliosajiliwa darasa la kwanza kulinganisha na waliofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka huu, hivyo wameanza kuwatafuta ili kufanya utafiti.

Prof. Mkenda aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya miaka 50 ya Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA). Baraza hilo lilianzishwa mwaka 1973.

"Bado sisi tunasikitika tunaangalia takwimu za wale waliojisajili darasa la kwanza halafu wakafanya mtihani wa darasa la saba mwaka huu, tumepoteza wanafunzi wengi, ile idadi hairidhishi. Kwa sisi tumeanza kwanza kuwatafuta kuangalia nini matokeo kisha tufanye utafiti," alisema.

"Hatuwezi kuvumilia kuona waliowaandikisha na bahati nzuri NECTA mnafanya vizuri mwanafunzi akiingia darasa la kwanza mnamweka kwenye mfumo wenu. Kwahiyo, akifika darasa la saba tutajua ni wangapi hawakufika darasa la saba.

"Tuna jukumu la kumweleza Rais Samia Suluhu Hassan tunafanya nini kama wizara na hilo tutalifanyia kazi, tukienda hivyo bila kufanyia kazi mfumo unaoruhusu mwanafunzi mwenye uwezo wa kimasomo kufanikiwa, utalalamikiwa," alisema.

Prof. Mkenda alisema wanapiga vita na kulaani wizi wa mitihani na kuwaomba Watanzania waendelee kuungana kukemea na kuadhibu wanaohusika.

Alisema serikali imechukua fedha Benki ya Dunia (WB) kujenga kampasi katika vyuo ambavyo vipo ili wazazi ambao hawataki watoto wao wasome mbali, wasome karibu nao.

"Tunajenga kampasi Tanga, Lindi, Kagera, Tabora, Kigoma, Singida, Njombe na Ruvuma. Tunaendelea na ujenzi na ukarabati wa shule kila mahali na shule za sayansi kila mkoa na ajira ya walimu zimeanza tena ili kila shule ipate fursa," alisema.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Mohamed, alisema katika miaka 50 ya baraza wamefanya mambo mbalimbali ikiwamo kongamano lililofanyika Visiwani Zanzibar lililowakutanisha wadau wa ndani na nje ya nchi kufanya tathmini ya mafanikio na changamoto katika sekta ya elimu.

Vilevile, alisema kuwa mwezi Oktoba walishiriki katika kuhamasisha jamii umuhimu wa utunzaji mazingira kwa kupanda miti katika shule mbili huko Mufindi ambako kuna kiwanda cha kutengeneza karatasi kwa kuwa baraza ni moja ya watumiaji wakubwa wa karatasi ambazo huzalishwa kwa kutumia miti. Pia alisema NECTA inaendelea na upimaji wa watoto katika kufikiri na kutenda kwa pamoja kwa kujiandaa kutekeleza mabadiliko ya Sera ya Elimu.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hashimu Komba, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, alisema NECTA inafanya kazi kubwa ya kuhudumia shule za msingi na sekondari ambapo Tanga inahudumia shule 1,381, Mwanza 1,368, Kilimanjaro 1,348 na Dar es Salaam shule 1,188.

Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya NECTA, Dk. Hassan Rashid Ali, akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wake, alisema wizara pamoja na shule binafsi zimewekeza kuhakikisha ufaulu katika shule unaongezeka.

"Nipongeze NECTA kwa kusimamia haki, uadilifu na utunzaji wa siri. Baraza linafanya kazi kama nyuki, hawalali. Tumepata hati safi. Tunaishukuru serikali kwa kuliwezesha baraza kutekeleza, shughuli zake," alisema.

**HABARI KITAIFA**

# Yabainika walengwa TASAF wanatumia 1,400/- kwa siku

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RIPOTI ya awali ya tathmini ya kipindi cha pili cha Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini, imeonesha kuwa katika kaya za walengwa, wastani wa matumizi kwa siku kwa mtu ni Sh. 1,419 kwa mwaka 2022, kiwango hicho ni chini ya mstari wa umaskini wa Tanzania Bara wa Sh. 1,859.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene (pichani), alibainisha hayo jana jijini hapa wakati akizindua ripoti hiyo.

Alisema matokeo yanaonesha pia wastani wa matumizi ya kaya moja ya mlengwa kwa mwezi ni Sh. 152,621; matumizi ya chakula yanachukua nafasi kubwa kwa Sh. 113,256, sawa na asilimia 74.2 ya matumizi yote ya kaya.

"Kiwango hiki cha matumizi ya kaya za walengwa kwa mwezi kipo chini kulinganisha na wastani wa matumizi ya kaya moja kwa mwezi nchini.

"Kwa msingi wa matokeo haya, ni dhahiri kuwa walengwa katika mpango wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) matumizi yao yako zaidi kwenye huduma ya chakula badala ya kuwekeza kwenye shughuli za uzalishaji ili kuongeza mtaji na kutoka katika hali ya umaskini iliyopo kwa sasa," alisema

Kutokana na hali hiyo, waziri huyo alisema serikali itaelekeza nguvu katika kaya hizo na kuhamasisha walengwa kuwekeza zaidi kwenye uzalishaji kwa lengo la kujiongezea kipato na hatimaye kutoka katika umaskini uliokithiri.

Alisema matokeo yanaonesha kuwa katika shughuli za uzalishaji, asilimia 50 ya kaya za walengwa zinajishughulisha na kazi za shamba la familia, asilimia 22 zinafanya kazi za malipo na asilimia 15 wamejiajiri wenyewe.

Alisema takriban asilimia 57 ya chakula katika kaya za walengwa huzalishwa na kaya zenyewe kwa matumizi yao wenyewe au kupewa zawadi kutoka kwa ndugu jamaa na marafiki na asilimia 43 iliyobaki ya chakula hununuliwa.

"Kwa matokeo haya, ninapenda kuhamasisha walengwa wa mpango wa TASAF kuhakikisha wanazalisha chakula kwa kutumia fursa zinazotolewa na serikali au wadau wengine katika maeneo wanayoishi.

"Kwa sasa mvua inayoendelea kunyesha nchi nzima, sote tutumie fursa ya kuotesha mazao ya muda mfupi kama mboga za majani, mahindi na mazao mengine kwa lengo la kujiongezea kipato,"alisema.

Kuhusu hali ya makazi, waziri huyo alisema matokeo yanaonesha kaya za walengwa zinaishi katika mazingira yasiyoridhisha.

Alisema 38 ya kaya za walengwa kuta za nyumba zimejengwa kwa udongo.

"Hapa niagize TASAF na viongozi wengine katika ngazi ya kata, kijiji na kitongoji kufuatilia kwa karibu mazingira wanamoishi hawa ndugu zetu na kutoa ushauri wa namna ya kujenga kwa gharama nafuu na kutumia vyombo vingine vya serikali kama Shirika la Nyumba la Taifa, nchi nyingine katika Bara la Afrika na duniani kote kundi hili hupewa kipaumbele katika



makazi wanamoishi.

"Serikali italifanyia kazi katika mpango mwingine unaofuata ili kuona ni kwa namna gani tunaweza kuwaweka hawa walengwa katika mazingira mazuri zaidi," alisema.

Kuhusu upatikanaji huduma za kifedha, matokeo yanaonesha asilimia nne ya walengwa wa mpango waliwahi kutembelea benki au taasisi nyingine rasmi ya fedha kwa ajili ya kufungua au kufunga akaunti.

Vilevile, alisema asilimia tisa ya kaya zina akaunti katika taasisi rasmi ya kifedha ikiwa ni pamoja na benki na taasisi ndogo za fedha.

Alisema katika sekta ya elimu, kiwango cha uandikishaji kwa elimu ya msingi ni kikubwa, asilimia 86 ya watoto katika kaya za walengwa wanahudhuria elimu ya msingi.

Alisema licha ya asilimia kubwa ya uandikishaji na mahudhurio, bado kiwango cha utoro kipo juu ambapo takriban asilimia 33 ya wanafunzi walikosa angalau siku moja kwenda shuleni katika wiki mbili zilizopita kabla ya siku ya utafiti.

Alisema matokeo yamebainisha kuwapo tofauti kubwa ya uandikishwaji wanafunzi kutoka kwenye kaya za walengwa kwa elimu ya sekondari.

"Asilimia 29 wanakaya wenye umri wa miaka 14-19 wanahudhuria shule ya sekondari na sababu kuu iliyotolewa na wakuu wa kaya ni ukosefu wa rasilimali fedha," alisema.

Kwa upande wa afya, alisema matokeo yamebainisha kuwa kaya za walengwa zinakabiliwa na matukio ya mara kwa mara ya kiafya.

"Takriban asilimia 65 ya kaya zilikuwa na mwanakaya ambaye alikuwa mgonjwa katika mwezi uliopita kabla ya siku ya utafiti na asilimia 45 ya wagonjwa hao walikwenda kupata matibabu katika kituo cha afya kilichoko karibu na wanapoishi.

"Nitoe wito hapa kwamba ni vyema unaposikia unaumwa uende kutibiwa katika kituo cha afya kilichopo karibu na unapoishi," alisema.

# Bosi mifumo ZEC atoa angalizo kwa waandikishaji wapigakura

**Na Suleiman Rashid**

MKUU wa Kurugenzi ya Mifumo ya Uchaguzi Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Mwanakombo Machano Abuu, amewataka wafanyakazi waliochaguliwa kuandikisha wapigakura wapya katika Daftari la Kudumu la Wapigakura, kuhakikisha kila mwenye sifa anaandikishwa na kuachana na ushabiki.

Amesema kazi hiyo iliyopangwa kufanyika wiki ijao kisiwani hapa, haihitaji ushabiki wa kisiasa.

Akizungumza na wafanyakazi hao waliopewa jukumu hilo kwenye ukumbi wa kiwanda cha mafuta ya Makonyo Wawi, Mwanakombo alisema uandikishaji utaanza katika Wilaya ya Micheweni.

Aliwataka kila mmoja kuelekeza akili yake katika kazi hio muhimu ya kitaifa kwa kuzingatia uadilifu na kumpa haki kila anayestahili kuandikishwa kwenye daftari hilo ili hatimaye awe miongoni mwa Wazanzibar watakaokuwa wapiga kura.

"Niwaombe sana jiepusheni na kushabikia vyama wakati wa uandikishaji kwani kufanya hivyo kunaweza kulitia dosari zoezi zima la uandikishaji," alisema Mwanakombo.

Aliwataka kufanya kazi hiyo kwa misingi iliyowekwa na maelekezo waliyopewa na kuacha kujiona kuwa wao ndio wenye akili zaidi ya walio wengi walioomba kazi hiyo, lakini wakaikosa. Walioomba ni wengi, lakini mahitaji ni machache.

Alisema waliohitajika walikuwa ni wakuu wa vituo 38 kwa Pemba na waandikishaji 76. Tume iliwachagua na kuwa amini, hivyo wawe na mrejesho mzuri kutokana na kuaminiwa kwao.

Alisema kufanya vizuri kwa waandikishaji hao ni pamoja na kutii maagizo waliyopewa ikiwamo kutunza vifaa, kutunza siri ya kazi waliyopewa na kujenga nidhamu itakayowasaidia kufanya kazi pasi na misuguano baina yao.

Alisema haitapendeza kumwona karani wa uandikishaji anachezea mifumo kwa shughuli ambazo hazihusiani na uandikishaji. Wamefundishwa kutumia vifaa vya tume vinavyohitaji uangalifu mkubwa.

"Ninaomba nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena kuwakumbusha kuwa mnakwenda kufanya kazi katika jamii tofauti. Cha msingi kwenu ni kuhakikisha mnatoa huduma bora ili sisi tuliowatuma tujifariji kuwa tume tuma watu wanaofaa," alisema.

Mwanakombo pia aliwataka watumishi hao kuwasimamia vyema watu wenye mahitaji maalum; wazee, walemavu na wajawazito ili nao wapate haki yao bila ya usumbufu.

Ofisa Uandikishaji ZEC Wilayani Chakechake, Abdalla Juma Abdalla, aliwataka waandikishaji hao kujenga ushirikiano na kutambua sifa za wanaotakiwa kuandikishwa.

ZEC inatarajia kuandikisha wapigakura wapya kwa awamu ya kwanza wiki ijayo katika Wilaya ya Micheweni ikiwa ni maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.


AFRICA PROPERTY LTD

*Valuers, Estate & Property Managing Agents, Land Development Consultants P. O Box 32822, Dar es Salaam & P.O Box 1250, Arusha, Tanzania*

## TENDER FOR SALE OF LANDED PROPERTIES

**AFRICA PROPERTY LIMITED** on behalf of our client is hereby advertising sale of the below listed landed properties by **TENDER.** The details of the properties are described below.

| S/N | DESCRIPTION OF PROPERTIES | LOCATION |
|---|---|---|
| 1.0 | Three (3) storey commercial building located on Plot No. 18, COMMERCIAL AREA (AREA E), ARUSHA CITY. (CT. NO. NP 35) The property is a 3 storey office building currently occupied by various tenants, including a reputable bank. | Goliondoi Street, Arusha City Centre |
| 2.0 | Land parcel located on Plot No. 34, COMMERCIAL AREA (AREA - E), INDIA STREET, ARUSHA CITY. (CT. NO. 975) The Land Parcel is currently used (temporarily) as a car parking ground. | India Street, Arusha City Centre |
| 3.0 | Land parcel located on Plot No. 21, COMMERCIAL AREA (AREA - E), ARUSHA CITY. (CT No. 9824) The land parcel is currently used (temporarily) as a car parking space. | Junction of Goliondoi and Makongoro Street, Arusha City Centre |

**TERMS AND CONDITIONS OF TENDER**

1. Interested buyers are advised to obtain further information of the properties from AFRICA PROPERTY LIMITED vide telephone numbers +255 754260864/0784260864/0754642141
2. Valuation, inspection, and Title Search reports of the properties shall be conducted by the interested buyers/bidders themselves prior to submission of the bids for purchase of the properties.
3. Electronically mailed and late submission of bid documents shall not be accepted.
4. Bid documents should be in plain envelope with the outer cover clearly marked. "TENDER NO. APL/CPL/01/2023 FOR PURCHASE OF LANDED PROPERTY." Addressed to AFRICA PROPERTY LIMITED as per below

   **Address:**
   **CHIEF EXECUTIVE OFFICER**
   **AFRICA PROPERTY LIMITED**
   **CENTRAL PLAZA, SECOND FLOOR, PLOT NOS. 71 & 72, ALONG SOKOINE ROAD**
   **P. O. BOX 1250**
   **ARUSHA**
   **TEL. NOS. 0754260864/0754642141**

5. Deadline for submission of the bid documents shall be on 11th December 2023 at 1:30 pm.
6. The tender documents shall be opened on 11th December, 2023 at 3:00 pm at AFRICA PROPERTY LIMITED offices located at CENTRAL PLAZA, SECOND FLOOR, PLOT NOS.71 & 72, Along Sokoine Road, Arusha.
7. The successful bidder shall be bound to make advance payment of 25% of the bid price by way of a Bankers' Cheque in favour of the seller or deposited into a Bank Account as shall be advised by the seller upon the successful bidder being announced as the successful bidder and the remaining 75% balance shall be paid within 14 days from the date of award.
8. If the remaining 75% will not be paid within 14 days, the buyer shall forfeit the advance 25% payment and the next highest bidder shall be awarded the option to purchase the property.
9. The seller shall not be bound to accept the highest bid if the bid price is lower than the reserve price.
10. Bidders wishing to view the property or inspect the property may do so subject to making an appointment with AFRICA PROPERTY LIMITED vide the telephone numbers indicated in item 1.0 above.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ajali za kila mara barabarani zipatiwe ufumbuzi wa kudumu

**AJALI** za barabarani zimeendelea kugharimu maisha ya watu huku baadhi wakipoteza maisha na wengine kujeruhiwa. Ndani ya siku tatu wiki hii, kwa mfano, ajali tatu zimetokea katika maeneo tofauti nchini na kusababisha watu 30 kufariki dunia na 72 kujeruhiwa.

Katika ajali ya kwanza iliyotokea Mtama mkoani Lindi Novemba 26, mwaka huu,ikihusisha basi la Baraka Classic linalofanya safari kati ya Dar es Salaam na Tandahimba mkoani Mtwara, watu 14 walipoteza maisha na 26 kujeruhiwa. Chanzo cha ajali hiyo, kwa mujibu wa Jeshi la Polisi ni basi kufeli breki.

Wakati gumzo la ajali hiyo likiwa bado linaendelea, juzi alfajiri Manyoni mkoani Singida, basi la Ally's Star likitoka Dar es Salaam kwenda Mwanza, liligonga injini ya treni na kusababisha watu 13 kupoteza maisha. Licha ya watu hao kufariki dunia, wengine 32 walijeruhiwa.

Kama vile haitoshi, usiku wa Novemba 29, mwaka huu, ajali nyingine ilitokea Mwanga mkoani Kilimanjaro iliyosababisha watu watatu kufariki dunia, akiwamo bibi harusi mtarajiwa aliyekuwa akiendesha gari aina ya Toyota Raum akiwa na mama yake mzazi na mfanyakazi wa ndani wakitokea Morogoro baada ya gari hilo kugongana na Scania ya mizigo.

Bibi harusi huyo alikuwa akienda kwa ajili ya kufunga ndoa iliyotarajiwa kufanyika kesho jijini Arusha.

Ajali hizo zilizotokea siku chache kabla ya kuingia mwezi wa mwisho wa mwaka, ni mwendelezo wa matukio kadhaa kama hayo yaliyotokea mara kadhaa kwa mwaka huu. Sababu zinazotolewa kuwa chanzo cha ajali hizo ni zile zile ambazo ni sawa na hadithi za alfu ulela ulela. Miongoni mwa sababu hizo ni uzembe wa madereva, kufeli breki, mwendokasi na kukosa umakini wawapo barabarani.

Kuwapo kwa ajali hizo Watanzania wakiwa kwenye maandalizi ya sikukuu za mwisho wa mwaka, ni ishara ya kuwaamsha wali-opewa dhamana ya usalama barabarani kuamka na kuchukua hatua, vinginevyo jamii itegemee maafa zaidi. Hiyo ni kutokana na watu wengi kutoka sehemu moja kwenda nyingine na katika safari hizo, uzoefu unaonyesha kwamba kumekuwa na ajali nyingi za barabarani ambazo hugharimu maisha ya watu ama vifo au majeruhi.

Wakati kama huu, huwa kuna taabu ya usafiri kutokana na magari kujaa hali ambayo husababisha Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) kutoa vibali kwa mabasi kama Toyota Coaster na yale yanayotoa huduma za usafirishaji katika mkoa wa Dar es Salaam, maarufu kama daladala.

Ni wakati mwafaka sasa kwa LATRA na Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani kuanza ukaguzi wa kina ili kuhakikisha magari yanayobeba abiria kutoka sehemu moja kwenda nyingine, hasa mikoa ya kaskazini ya Kilimanjaro na Arusha, ambako kuna utamaduni wa watu kukusanyika kifamilia kusherehekea Krismasi na Mwaka Mpya.

Kwa ujumla, kama alivyosema Rais Samia Suluhu Hassan kuwa amechoka kutoa pole na salamu za rambirambi kutokana na ajali za barabani zinazotokea mara kwa mara, ufike wakati sasa hatua kali zichukuliwe dhidi ya wamiliki na madereva ambao magari yao yanasafirisha abiria yakiwa hayana ubora na viwango.

Ni dhahiri kwamba ziko hatua ambazo zimekuwa zikitangazwa kuchukuliwa zikiwamo madereva kufungiwa leseni na magari kusitishiwa vibali vya utoaji wa huduma. Kwa mtazamo yakinifu, inaonekana kwamba adhabu hizo bado ni ndogo ndiyo maana ajali zimekuwa zikiendelea, hivyo ni wakati mwafaka wa kutunga sheria kali ambazo zitawaumiza wahusika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hongera benki ya wana- kilimo kwa kuwakumbuka wahusika kuwakopesha

Na Halfani Chusi

**HONGERA** benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), kuamua kuwakopesha wakulima kwa lengo la kuwatoa kutoka kilimo cha kujikimu mpaka kilimo biashara yaani hatua moja kwenda nyingine.

Ni msimu mwingine wa kilimo, ambao wakulima wanajiandaa na kilimo cha kutegemea mvua na wengine kile cha umwagiliaji hata hivyo wanajikuta katika tabasamu kwamba ipo nguvu ambayo ni benki ya (TADB), inasimama kama mbadala pale wanapokwama.

Ni aina ya huduma inayotia faraja na kuongeza hali ya ufanyaji kazi kwa wakulima. Hata hivyo, wanaushauri kwa wakulima nchini wajiunge na vyama vya ushirika vya kilimo ili waweze kunufaika na huduma ya mikopo hiyo kwa kuwa kipaumbele cha kwanza cha utoaji wa mikopo yao ni kwa wale waliojiunga katika vyama vya ushirika.

Nilishuhudia siku chache zilizopita mkoani Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi wa Mipango na Utafiti benki hiyo, Mkani Waziri, akizungumza na Ushirika wa Mwamapori AMCOS kutoka Tabora Igunga, walioenda kwake kwa kutembelea vyama vingine vya ushirika ili kujifunza namna walivyofanikiwa kupitia mikopo hiyo.

Alisema lengo la benki hiyo ni kutoa huduma za mikopo kwa wakulima na zile zisizo za mikopo, kama vile kuwapa mafunzo wanaokopa ili waweze kupiga hatua kimaisha na kuipaisha nchi kiuchumi.

Katika kikao hicho, aliwakumbusha wakulima hao kuwa jukumu kubwa walilopewa na serikali, ni kuhakikisha nchi inajitosheleza kwa usalama wa chakula, pamoja na kuwasaidia wakulima kupiga hatua kutoka kilimo cha chakula hadi kufikia cha kujikimu.

"Kazi ya benki hii ni kuleta suluhisho kwenye kilimo, tunakwenda mikoani kuwatembelea wakulima wengine tunaamini huko tutajifunza kutoka kwao na wao watajifunza kutoka kwetu ili kutanua wigo wa uzalishaji.

"Benki hii inaangalia maendeleo ya mteja wake, serikali itatupima kwa kuangalia tumefanya nini kwa wakulima na sisi hatuangalii sana kulipwa deni, bali tunaangalia mkulima amefaidikaje na mkopo" anasema Waziri.

Alisema, huduma inayotolewa na benki yao kwa sasa, imewafikia wakulima nchi nzima akisisitiza kuwa ofisi zao zimejigawa kikanda nchi nzima na kwamba walengwa ni wavuvi, wafugaji na wakulima.

Ni jambo linaloungwa mkono na Mkuu wa Kitengo Cha Sheria, Dk Edson Rwechungura anapozitaja njia wanazotumia kuwafikishia wateja wao mikopo kuwa ni pamoja na kushirikiana na benki nyinginezo mbili, kwa kudhamini wanayopewa wakulima nchini kote.

"Mpaka sasa tumedhamini mikopo ya bilioni 228, kwa wakulima ambao wengi wamenufaika na wamekiri imewabadilishia maisha yao," alisema

Ramadhani Muna, Mwenyekiti wa Ushirika unaoitwa Mwamapori,ulioko Igunga Tabora, kwa niaba ya wakulima ambao wananufaika na mikopo ya benki hiyo aliishukuru benki hiyo kwa kuwainua wakulima akibainisha mikopo wanayopewa imeleta tija.

"Sisi wanaushirika tupo 970 lakini tuliotoka Tabora kuja hapa Dar es Salaam kwa ajili ya kuanza ziara ya kutembelea washarika wengine tupo 10 kwa ajili ya kupata mafunzo na kujifunza kwa kuwatembelea wengine baada ya hapo tutakwenda kuwa mabolozi kwa waliobaki na kuwapa elimu ya kile tutakacho kiona kwenye ziara," alisifu.

Ni jambo zuri wakulima kuwezeshwa kupewa mikopo, hii itasaidia kuinua maendeleo ya nchi na kukuza uchumi wetu kwa kasi, kinachofanywa na benki hiyo kinapaswa kuigwa pia na benki nyingine ili huduma hiyo iweze kufanyika kwa haraka na kuwafikia wakulima nchi nzima.

## HABARI KITAIFA

# Wadau: Mifumo mikataba kimataifa iboreshwe

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa sheria nchini wameishauri serikali kuweka mifumo ya wazi na shirikishi ya kusimamia mikataba ya kimataifa ili kuepuka kulipa madeni yatokanayo na kukiuka au kuivunja mikataba hiyo hali inayochangia kuirudisha nchi nyuma kimaendeleo.

Walisema maboresho hayo yatasaidia kuwapo kwa uwajibikaji, uwazi na kuongeza umakini kwa watendaji na wawekezaji katika mchakato mzima wa utekelezwaji wake na kupunguza migogoro inayosababisha kusitishwa na kulitia deni taifa.

Waliyasema hayo mjini Dodoma wakati wakitoa mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu Mikataba ya Uwekezaji ya Kimataifa yaliyoandaliwa na Mtandao wa Muungano wa Asasi za Kiraia zinazofanya Uchambuzi wa Sera za Uwekezaji na Biashara Tanzania (TATIC).

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Cha Sheria Tanzania, Clement Mashamba, alisema maboresho ya mifumo hiyo itasaidia kuwapo uratibu wa karibu na usimamizi mzuri wa mikataba hiyo tangu inaposainiwa hadi utekelezaji wake. Alisema ili suala hilo lifanikiwe kunatakiwa maboresho hayo yatambulike kisheria ili wasimamizi na wawekezaji wayazingatie wakati wa utekelezaji wa mikataba hiyo.

Pia alishauri kuwapo na bajeti ya kutosha kukiwezesha kitengo cha uratibu wa mikataba ya kimataifa kufanya kazi hiyo na watu wake waongezewe maarifa kuhusu utekelezaji na usimamizi wa mikataba hiyo ili wawe na weledi.

"Mifumo hii pia itasaidia kunapotokea migogoro, timu zitaweza kuangalia namna bora ya kuitatua kulingana na aina ya mkataba na athari zake kwa nchi," alisema.

Mjumbe wa Bodi ya TATIC, Wakili Stephen, Msechu, alisema kama mifumo iliyopo ikiboreshwa, itaiepusha nchi na hasara zitokanazo na kulipa fidia kampuni zinazokuja kuwekeza nchini kwa kuingia mikataba ya kimataifa ambayo inawalinda.

Alisema kwa miaka ya hivi karibuni nchi hiyo imepoteza takribani Sh. trilioni 1.5 kwa kesi chache zinazofahamika zilizotokana na kukiuka mikataba hiyo, pesa iliyotokana na kodi za wananchi.

Alisema mifumo hiyo inatakiwa ifuate hatua zote bora za kusimamia mikataba ya kimataifa ikiwamo kuwapo sheria mahususi ya kuisimamia na inayoelekeza nani atie saini mikataba hiyo kama ilivyofanya nchi ya Uganda.

Alishauri pia kuongeza nguvu katika mifumo ya uratibu na ufuatiliaji wa mikataba hiyo, utakaoshirikisha taasisi zote husika ili kwa pamoja kumbana mwekezaji anayelindwa na mikataba hiyo.

"Kimsingi bila kuweka mifumo ya wazi na shirikishi ya kusimamia hii mikataba bado tutaendelea kuikosea na kuwajibishwa kwa kulipa fidia baada ya kushtakiwa kwenye mahakama za mikataba," alifafanua Wakili Msechu.

Mkurugenzi Mtendaji wa TATIC, Olivia Balilo, alisema wametoa mafunzo hayo kwa waandishi wa habari ili kuwajengea uwezo kuhusu athari chanya na hasi za mikataba hiyo kwa nchi ili wanapoandika habari wawe na uelewa mpana.

Alisema vyombo vya habari vina uwezo wa kufikia jamii pana zaidi, wameona waongeze wigo wa kufikisha elimu ya mikataba hiyo kwa jamii kupitia vyombo hivyo kwa kuwapa mafunzo.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila (kushoto), akisalimiana na Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Maendeleo TIB, Agapiti Kobello (wapili kushoto), wakati alipowasili kufungua Mkutano wa Wadau wa benki hiyo, Kanda ya Dar es Salaam uliofanyika jijini humo, jana. Wengine ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki hiyo, Juma Reli (watatu kushoto), Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TIB, Lilian Mbassy (wapili kulia) na Kaimu Mkurugenzi wa Usimamizi wa Miradi, Zuwena Hemed. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dk. Tulia Ackson aiagiza kamati ya IPU kushughulikia mgogoro Israel, Palestina

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Dk. Tulia Ackson, ameielekeza Kamati inayoshughulikia Masuala ya Mashariki ya Kati ya Umoja huo kutembelea eneo hilo mapema katika juhudi za kutafuta suluhisho linaloweza kuhakikisha amani na usalama vinapatikana kutokana na mgogoro unaoendelea baina ya Israel na Palestina.

Dk. Tulia aliyasema hayo jana, jijini Tel Aviv nchini Israel baada ya kumaliza ziara yake ya kikazi ya siku mbili iliyompa fursa ya kukutana na kufanya mazungumzo na viongozi mbalimbali wa Israel na Mamlaka ya Palestina.

"Nimekuja kutembelea maeneo ya Palestina na Israel ambao wote hawa mabunge yao ni wanachama wa IPU, lakini muhimu zaidi kuwafahamisha kuwa tupo pamoja nao katika kipindi hiki kigumu na kamati yetu inayoshughulikia Masuala ya Mashariki ya Kati itakuwa hapa siku zijazo kutafuta uhalisia wa mgogoro huu na kuleta taarifa ambayo tutapata nafasi ya kuijadili ili tuone huko mbele tunakokwenda tunawezaje kuwa na amani na usalama kwa watu wote," alisema Dk. Tulia.

Alifafanua kuwa, moja ya msingi wa IPU ni kuhakikisha uhai wa kila binadamu unalindwa na utafanya kila linalowezekana ili dunia iwe sehemu salama na ya amani kwa binadamu wote bila kujali rangi, itikadi, imani na maeneo wanayotoka.

Aidha alisisitiza kuwa, mpango mkakati wa Umoja huo ni kuutumia mwaka 2024 pamoja na mambo mengine kujadili kwa kina suala la amani na usalama kama ajenda muhimu kwenye mikutano yake mikuu ya mwezi Machi na Oktoba, mwakani.

Katika ziara hiyo Dk. Tulia na ujumbe wake amekutana na kufanya mazungumzo na viongozi wa Mamlaka ya Palestina jijini Ramallah akiwamo Waziri Mkuu wa Mamlaka hiyo, Muhammad Shtayyeh na Spika wa Baraza la Mamlaka ya Palestina, Rawhi Fattouh.

Vilevile, Dk. Tulia alipata fursa ya kutembelea Kijiji cha Kfar Aza Kibbutz kati ya vijiji vilivyoshambuliwa na wanamgambo wa Hamas Oktoba 7, 2023 na kufanya mazungumzo na Spika wa Bunge la Israel (Knesset), Amir Ohana, Waziri wa Kilimo na Maendeleo ya Vijiji, Avi Dicter na wabunge wawakilishi wa Knesset kwenye IPU walioongozwa na Danny Daddon.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# Wahasibu, wakaguzi watakiwa kuboresha taaluma

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amewataka wahasibu na wakaguzi wa hesabu nchini kuendelea kuboresha taaluma yao ili wafanye kazi kuendana na kasi ya ukuaji wa teknolojia ya dijitali.

Kadhalika, amewataka kuzingatia maadili katika kutekeleza majukumu ya kila siku.

Alitoa kauli hiyo wakati akifungua kongamano la siku tatu la Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA) linalofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema taaluma pekee haitoshi bali pia kuwa na sifa na ujuzi muhimu katika kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha na weledi ikiwamo kuzingatia maadili na uwajibikaji katika kazi hiyo.

"Taaluma si tu kuwa na sifa na ujuzi muhimu, bali pia kuhusu kuwa na viwango vya juu zaidi vya maadili, uwajibikaji na kuendelea kuboresha zaidi ujuzi na kuendana na kasi ya ukuaji wa teknolojia. Kama wanataaluma hii, mnapaswa kuhakikisha uwapo wa afya ya kifedha na utulivu wa wadau wako na muhimu kulinda imani ambayo jamii imeweka kwako," alisema Simbachawene.

"Taaluma ya uhasibu ni mojawapo ya nguzo muhimu ambazo zinahitajika katika karibu nyanja zote. Kwa hiyo ili kufikia ukuaji na maendeleo endelevu, uboreshaji wa kitaaluma haupukiki. Wahasibu wa kitaaluma wanapaswa kufanya jitihada za kuongeza sifa zao, ujuzi na tabia zinazohusiana na taaluma yao."

Mwenyekiti wa Bodi hiyo ya NBAA, Prof. Sylivia Temu, alisema katika kongamano hilo, washiriki watajadili mambo mbalimbali ikiwamo namna CPA inavyotakiwa kufanya vizuri katika ulimwengu wa kidijitali, nafasi ya wahasibu na wakaguzi wa hesabu katika maendeleo ya nchi.

Temu alisema kuna haja kwa wahasibu kuendeleza uwazi wa kifedha, kuimarisha uwajibikaji na kufanya uamuzi sahihi ndani ya mashirika yao.

Pia, alisema wahasibu ni washauri muhimu wa masuala ya kifedha ni muhimu wao kufanya kazi kwa weledi zaidi kuleta maendeleo kwenye taasisi zao na kuzingatia weledi na maadili, uadilifu ni muhimu kwao.

Mkurugenzi Mtendaji wa NBAA, Pius Maneno, alisema kongamano la mwaka huu linalenga kuongeza zaidi nguvu katika taaluma hiyo kwa kufanya mageuzi kuelekea maendeleo endelevu.

"Na Tanzania tunakwenda sambamba na mwelekeo wa kimataifa wa uhasibu kwa kufuata kanuni bora za kimataifa za uhasibu kwa maendeleo endelevu," alisema.



Mkurugenzi wa Miradi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Mhandisi Ramadhani Mtindasi (mwenye kipaza sauti), akitoa maelezo kwa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha (AUWSA), kuhusu mradi wa maji Kigamboni walipotembelea miradi ya mamlaka hiyo, jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Watumishi watimuliwa kazi tuhuma ulevi uliokithiri

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, limewachukulia hatua watumishi wanane wa halmashauri hiyo, baadhi yao kufukuzwa kazi kutokana na tuhuma mbalimbali ikiwamo kushindwa kutekeleza majukumu kutokana na ulevi uliokithiri.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, James Mkwega, alitangaza uamuzi uliofikiwa na baraza hilo jana wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani kilichoketi kwa ajili ya kujadili utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024.

Aliwataja waliofukuzwa kazi kuwa ni wauguzi wawili, Antonia Atanasi ambaye ni Mtabibu msaidizi Zahanati ya Mziba na Mary Kingu, ambaye ni muuguzi wa Zahanati ya Iguguno.

Watumishi hao wamechukuliwa adhabu hiyo kutokana na kosa la utoro kazini kwa zaidi ya siku tano bila taarifa ya mwajiri.

Mkwega aliwataja watumishi wawili waliochukuliwa adhabu ya kukatwa mshahara kwa asilimia 15 kwa muda wa miaka mitatu kutokana na ulevi uliokithiri kuwa ni Kelvin Nyachi ambaye ni Ofisa Ununuzi Msaidizi, Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama na Farida Mathias Kigaila ambaye ni mteknolojia mwandamizi wa maabara katika Hospitali ya Wilaya ya Mkalama.

Watumishi wengine waliopewa barua ya onyo kwa kosa la kukiuka taratibu za fedha na ununuzi ni Ismail Tundu, Ofisa Mtendaji kijiji na Daudi Mazengo, Mtendaji wa Kijiji cha Manyongo.

Mtumishi mwingine aliyechukuliwa hatua ni Mtatiro Galache, Mteknolojia wa dawa, kituo cha afya Nyabuli aliyepewa adhabu ya kukatwa mshahara kwa asilimia 15 kwa muda wa miaka mitatu.

Pia Mizungu Macheli Chazy Mtabibu msaidizi hospitali ya Wilaya ambaye alikuwa akituhumiwa kwa ulevi, Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama liliamuru tuhuma zake zichunguzwe upya.

Mkwega akizungumza baada kusoma uamuzi huo wa baraza, alisema madiwani hawafurahii kumwita mtumishi kwenye kamati ya uongozi kuhojiwa kwa ya ulevi.

Aliwataka watumishi wazitendee haki nafasi zao kwa kuwa kuna watu wanaoenda kwa waganga wa kienyeji na wengine kwenda na udongo na maji kuombewa ili wapate nafasi za kuteuliwa, lakini hawakufanikiwa.

"Mwaka 2014/2015 haikutokea kujadili mtumishi yeyote kwenye Kamati ya Uongozi, lakini leo hii inatokea mtumishi anajadiliwa kunywa pombe halafu haijakatazwa kunywa kinachotakiwa usinywe wakati wa kazi," alisema.

# DAWASA yapongezwa matumizi TEHAMA

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imepongezwa kwa kuweka kipaumbele matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira ndani ya eneo lake la kihuduma imekuwa ya mafanikio makubwa.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Arusha (AUWSA), Mhandisi Dk. Richard Masika, wakati bodi hiyo ilipofanya ziara ya mafunzo DAWASA na kubadilishana uzoefu.

Mhandisi Masika aliipongeza DAWASA kwa utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayolenga kuboresha upatikanaji wa majisafi pamoja na kuleta mapinduzi katika teknolojia kupitia matumizi ya TEHAMA.


"Katika ziara yetu tumevutiwa zaidi na matumizi ya TEHAMA katika ukusanyaji wa taarifa, uhakiki wa taarifa pamoja na uanzishwaji wa kitengo cha kudhibiti upotevu wa maji ambacho kimetajwa kuwa msaada mkubwa kwa Mamlaka," alifafanua.

Mhandisi Dk. Masika alitoa rai kwa mamlaka zingine za maji nchini kuandaa ziara za mafunzo kutembelea DAWASA kwa sababu imepiga hatua kubwa katika uendeshaji na utekelezaji wa miradi mikubwa.

Awali, wakati akiwasilisha taarifa ya mamlaka, Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi DAWASA, Lanston Msongole, alisema mamlaka hiyo inatekeleza shughuli zake mbalimbali kwa kutumia mifumo ya TEHAMA ili kuendana na mapinduzi makubwa ya teknolojia duniani pamoja na ongezeko kubwa la idadi ya watu.

"Pamoja na kutekeleza miradi ya maji na usafi wa mazingira kwa mafanikio makubwa, DAWASA pia inajivunia mapinduzi makubwa katika sekta ya TEHAMA ambayo imerahisisha utoaji wa huduma pamoja na mawasiliano kati ya mteja na mamlaka," alisema.

Ziara ya wajumbe wa bodi ya wakurugenzi AUWSA imehusisha kupokea taarifa ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya majisafi na usafi wa mazingira pamoja na kutembelea mradi wa maji Kigamboni uliotekelezwa na DAWASA kwa gharama ya Sh. bilioni 25.







Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (aliyechuchumaa kulia), akimsikiliza mkazi wa Kata ya Bassotu, wilayani Hanang', Ezekia Samo wakati akiwa kwenye kampeni yake ya kusikiliza jamii ya vuta pumzi, funguka, ongea na mkuu wa mkoa, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Kaburi la mwanamke anayedaiwa kuuawa na wasiojulikana lafukuliwa

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

KABURI la mwanamke mwenye asili ya Kiarabu, anayedaiwa kuuwawa na watu wasiojulikana na kuzikwa kwenye eneo la mwekezaji Mtaa wa Mafuriko, Kata ya Mzizima, Jijini Tanga, limefukuliwa na serikali.

Baada ya kufukuliwa kaburi hilo, mwili wa marehemu haukuwepo, bali kulikutwa mayai viza, nazi pamoja na vitambaa vyeusi.

Mkuu wa Wilaya ya Tanga, James Kaji, alifika eneo hilo alisema mara baada ya kupata taarifa kutoka kwa wananchi walichukua hatua za kulifukua kwa kibali cha mahakama na kukuta sanda nyeusi, nazi tatu na yai viza ishara ya Imani ya kishirikina.

"Ni kaburi ambalo lilionekana lipo ndani ya eneo la mwekezaji, lakini wakati tunaendela na ufukuaji tumekuta wananchi wengi wamevamia eneo hilo ambalo limepimwa viwanja kwa kisingizio kwamba hawana maeneo ni kana kwamba wametengeneza tukio hilo ili kumtisha mwekezaji " alisema.

Kaji alipiga marufuku ya kutoonekana kwa mtu yeyote katika eneo hilo na kusema kuwa kumekuwa na tabia ya wananchi kuvamia maeneo ya wazi na baadaye kuomba fidia kwa serikali.

Alibainisha kwamba wananchi wamezoea kujichukulia maeneo na kuweka makazi ya kudumu na inapotokea serikali inayahitaji wanakimbilia kwa wanasiasa kupata msaada ambao hutumia kama mwanya wa kuombea kura.

Alisema tabia hiyo imekuwa na imekuwa ikiiletea serikali matatizo makubwa ya migogoro ya ardhi ambayo mara nyingi hutokana na uvamizi wa wananchi kwenye maeneo yenye hati miliki.

Mmoja wa mashuhuda, Yusuf Mwinjuma alisema aliona mwili wa mwanamke huyo ukizikwa lakini anashangazwa na kutokuwapo dalili zozote zinazoonesha kama alizikwa hapo na kwamba bado hawaamini kwa kilichotolewa ndani ya kaburi hilo.

"Cha kushangaza ni kwamba, watu waliamini kwamba marehemu alizikwa kaburini humo, sasa hivi vitu vilivyotolewa hapa siyo vya kawaida kabisa, imani iliyojengeka ni kuhusu ushirikina jambo ambalo kwakweli limetuletea taharuki na hofu," alisema Yusuf Mwinjuma.

# Serikali yapata mwarobaini vishoka upimaji ardhi, ramani

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

KILIO cha muda mrefu kuhusu ubabaishaji wa vishoka katika tasnia ya wapima ardhi na ramani nchini, kimepata majibu, baada ya serikali kutangaza mfumo mpya wa 'ardhi kiganjani' utakaowawezesha kuepuka usumbufu na kutapeliwa.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geoffrey Pinda, alitangaza mfumo jana, katika mkutano mkuu wa mwaka wa wapima ardhi nchini uliofanyika Arusha.

Aliiagiza Taasisi ya Wapima Ardhi na Ramani Tanzania (IST), kutumia mfumo huo kuwadhibiti vishoka wanaotembelea kivuli cha taaluma hiyo nchini, ambao hawana weledi pamoja na wale wanaokiuka maadili ya taaluma yao.

Vilevile ameitaka kuchukua hatua haraka kama mwarobaini wa kukabiliana na migogoro ya ardhi isiyokoma.

"Wizara yenu kwa sasa, inajenga mfumo wa TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) utakaowawezesha kuwa na ardhi kiganjani, yaani Ardhi App, ambayo itatengeneza tiba ya kudumu kwa Watanzania kuwa na ardhi yao kiganjani ili kuondoa vishoka wanaosababisha migogoro ya ardhi,"alisisitiza Pinda

Aliwaelekeza wadau waliohudhuria mkutano hao kujitafakari na kuweka mikakati ya kuwadhibiti watu wachache wanaochafua taaluma hiyo kwa kukiuka maadili ya kazi.

"Wakati umefika wa kupitia chombo chenu, kubaini changamoto zinazowakabili, kwa sababu Wizara yenu ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inatishiwa na migogoro mingi ya ardhi inayoonyesha udhaifu wenu katika kusimamia."

Naibu waziri Pinda, alisema kila kona ya nchi, kuna vilio vya migogoro ya ardhi ikiwemo mwingiliano wa mipaka kati ya kijiji na kingine, kata na kata, wilaya na wilaya na hata mkoa kwa mkoa, kwa sababu ya IST kukosa umakini.

Hata hivyo, amewapongeza wataalamu hao kwa kuchangia maendeleo ya nchi kupitia miradi mikubwa na midogo, ingawa wanakabiliwa na changamoto ya vitendea kazi vya kisasa na ofisi.

Kwa mujibu wa Pinda, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Ardhi (NLUPC), imeonyesha mafanikio makubwa katika uwekaji wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji na suluhisho ya mipaka.

Katika mkutano huo, Rais wa IST, Tryphon Bilauri, aliiomba serikali kuharakisha mchakato wa kufanyia mabadiliko ya sheria mbili, zinazoongoza taaluma hiyo, ambazo ni sura, namba 324 na namba 270 ya mwaka 1977, kwa kuwa kwa sasa zimepitwa na wakati.

Alisema mabadiliko ya sheria hizo yataendana na matumizi ya teknolojia ya upimaji ardhi na kuandaa ramani hivyo kuipa meno taasisi yao ya kuchukuliana hatua za kisheria.

## Wavumbuzi waitwa kujisajili BRELA

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKALA wa Usajili wa Biashara na leseni (BRELA), amewaelekeza wavumbuzi wa vifaa, dawa na bidhaa zingine kuhakikisha kabla havijatumika katika jamii, kuisajili kwao, ili kuepuka kushitakiwa kwa kuvunja sheria za nchi.

Akizungumza na wafanyabiashara wa jijini Arusha jana , Msajili Msaidizi wa BRELA, Benedictson Byamanyilwowa alisema wameamua kuzunguka maeneo mbalimbali nchini, ili kutoa elimu ya Hataza (uvumbuzi) kwa wafanyabiashara ili kuwaepusha na usumbufu wa kisheria.

Alisema dunia kwa sasa inaishi kwa teknolojia na uvumbuzi, hivyo wapo baadhi ya watu wanavumbua vifaa au dawa mbalimbali vinavyotatua matatizo mengi katika jamii na kuanza kuvitumia sokoni au katika jamii bila kusajili BRELA.

"Sasa ukianza kutumia sokoni au katika jamii ni kosa kubwa kisheria na ukibainika hatua zipo kali za kisheria za kukuchukulia, sasa tumeamua kuja kutoa elimu hii ni laima unapovumbua kitu chochote iwe kifaa, dawa na vingine vingi lazima uje kwetu usajili,"alisema.

Aidha alisema mtu anaposajili dawa, au kifaa chake anakilinda kisheria na kupata manufaa mengi ya kulindwa kisheria, tofauti na anapotumia bila kusajili.

Naye Ofisa Msajili BRELA, Julieth Kiwelu, alisema wapo Arusha kutoa elimua kwa ajili ya kuongezea uwezo wafanyabiashara, ili watumie bunifu zao katika biashara zao.

Ofisa Biashara wa Chama cha Wafanyabiashara Mkoa wa Arusha,Charles Makoi, aliishukuru BRELA kwa kuwapatia elimu hiyo ambayo itawasaidia kufanyabiashara kwa kufuata sheria na kuepuka ufanyaji biashara kimazoea.

"Pia unapovumbua au unapobuni kitu chako ni muhimu kusajili,vinginevyo mwenzako anapofahamu hujasajili, anatumia mwanya huo kwa kuja kusajili haraka BRELA na inakua haki yake, wewe unapokwenda kutaka kusajili umechelewa, matokeo yake unaanza kusumbuana na kesi miaka mingi bila mafanikio," alisema.



## HABARI KANDA YA ZIWA

# Bil.6.6 kumaliza adha ya maji vijiji 13 Kishapu

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MRADI mkubwa wa Maji kutoka Ziwa Victoria wa Igaga unaotekelezwa wilayani Kishapu kwa gharama ya Sh.bilioni 6.6 unatarajiwa kuondoa adha ya upatikanaji Maji safi na salama katika vijiji 13 wilayani hapa na kuhudumia zaidi ya wananchi 49,960.

Meneja wa Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Kishapu, Mhandisi Dickson Kamazima, alieleza hayo juzi wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo kufuatia ziara ya wabunge wa Jimbo la Kishapu na Umoja wa wanawake Tanzania (UWT) kukagua utekelezaji wa miradi ya maji jimboni humo.

Alisema miradi yote ya maji inayotekelezwa wilayani hapa ikikamilika upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi utafikia asilimia 65 hivyo kuondokana na adha ya kutumia maji yasiyo salama ya kwenye visima.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Juliety Payovela, alisema watahakikisha miradi yote ya maji inayotekelezwa mkoani humo inasimamiwa kwa makini na kukidhi mahitaji ya wananchi ili kutimiza dhamira ya serikali ya kumtua mama ndoo kichwani.

Mbunge wa Jimbo la Kishapu, Boniphace Butondo, alipongeza RUWASA kwa kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji wilayani humo, ambapo awali hali ilikuwa mbaya kwa wananchi kutumia maji machafu, lakini sasa shida hiyo imepungua kwa kiasi kikubwa.

Mbunge wa Viti Maalum mkoani Shinyanga, Santiel Kirumba, alisema hali ya utekelezaji miradi ya maji wilayani humo inaridhisha na kuwasihi wananchi kutunza miradi hiyo ili iendelee kutoa huduma kwa muda mrefu.

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Shinyanga, Grace Bizuru, alisema katika mradi huo wanajivunia ni kuona wanawake wenzao wakiondokana na adha ya shida ya maji iliyosababisha migogoro ya ndoa kwa baadhi yao.



Timu ya Wakurugenzi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, wakipata maelezo kuhusu mradi wa kilimo biashara ulioanzishwa na Mgodi wa Barrick North Mara, kwa ajili ya kuwawezesha vijana katika kijiji cha Nyangoto, wilayani Tarime, walipofanya ziara ya kikazi mgodini hapo jana na kutembelea miradi ya kijamii inayotekelezwa na mgodi huo. Wengine ni baadhi ya vijana wanufaika wa mradi huo na wafanyakazi wa mgodi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi walilia usafiri wa uhakika Mwanza-Ukerewe

**Na Rose Jacob,** UKEREWE

WANANCHI waishio katika kisiwa cha Ukerewe mkoani Mwanza, wamelalamikia hali ya ukosekanaji wa huduma za usafiri wa uhakika kutoka Nansio kwenda jijini Mwanza, tatizo linalodaiwa kushusha uchumi katika kisiwa hicho na visiwa jirani.

Wakizungumza na mwandishi wa gazeti hili kwa nyakati tofauti visiwani humo, wananchi hao waliiomba serikali kuingilia kati shughuli za utolewaji huduma za meli ili watoa huduma binafsi wafuate utaratibu wa kisheria.

Shida Mateo Mkazi wa Kijiji cha Bwishya kata ya Ukara wilayani humo alisema utoaji wa huduma za usafiri wa meli kwa sasa umekuwa na ratiba zisizoeleweka kutokana na watoa huduma binafsi kufanya jinsi wanavyojisikia bila kufuata utaratibu uliopo.

"Kama serikali inashindwa kusimamia ipasavyo ni bora ilete yenyewe usafiri wa uhakika ili tuache kubabaishwa babaishwa na watu binafsi,mbona maeneo mengine huduma ni nzuri ,tunaomba tuangaliwe,"alisema Mateo.

Alisema wanapata hasara kwenye biashara kwa kukosa huduma za usafiri hali inayowalazimu kuingia gharama tena za kulala na ulinzi wa mzigo pamoja na chakula na kusababisha hasara katika biashara zao.

Diwani wa Kata ya Kagunguli, George Nyamaha, alisema awali walikuwa na Meli nne ambazo ni MV Nyehunge,Mbijili,MV Urafiki ambazo ni za watu binafsi lakini zimekuwa zikisitisha huduma bila taarifa kwa abiria na MV.Butiama ya serikali, ambayo kwa sasa ipo kwenye matengenezo.

"Licha ya uhaba huo wa usafiri ambao umekuwa kero kwa wananchi vilevile Meli binafsi zimekuwa zikipandisha gharama za usafiri kiholela na utatuzi wa kero hii ni serikali kuleta meli ya uhakika italayoweza kubeba abiria,mizigo na magari," alisema Nyamaha.

Akizungumzia adha hiyo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ukerewe, Joshua Manumbu, aliwataka wananchi kuwa wavumilivu wakati meli za serikali zinapokuwa kwenye matengenezo ili kuepusha yasije kujitokeza madhara kama ya MV Nyerere.

Alisema kwa muda mrefu usafiri katika visiwa vilivyopo Ukerewe umekuwa wa shida,hivyo wanaishukuru serikali kwa kuwaletea kivuko cha Bukondo na Bwiro pamoja na kufanya tathimini ya kuweka kivuko cha Irugwa Kitale,Ghana na Kakukuru hali itakayomaliza kabisa tatizo la usafiri visiwani humo.

# Uwanja wa ndege Ibadakuli kukamilika Oktoba, 2024

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

MENEJA wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Mibara Ndirimbi, amesema Uwanja wa Ndege wa Mkoa wa Shinyanga Ibadakuli utakamilika Oktoba 3,2024 na kuongeza fursa za biashara mkoani humo.

Mhandisi Ndirimbi alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ziara ya vyombo mbalimbali vya Habari mkoani hapa baada ya ukaguzi wa ukarabati na ujenzi wa uwanja wa ndege na kusema ukarabati wake unafanyika kwa kipindi cha miezi 18.

Alisema Uwanja huo unakarabatiwa na kujengwa na Mkandarasi China Henan International Cooperation Group Co.Ltd (CHICCO) kwa gharama ya Sh. bilioni 44.8 huku mhandisi wa vifaa na ushauri ikiwa ni kampuni ya SMEC International L.t.d.

"Ujenzi wake ulioanza mwezi Aprili 2023 unaendelea vizuri kwa sasa umefikia asilimia 50 na kwa muda uliobaki tunaimani ifikapo Oktoba 3, 2024 utakuwa tayari umekamilika ili wananchi na wafanyabiashara waache kufuata huduma hii mkoani Mwanza na pengine kusafiri muda mrefu kwenda Dar es Salaam," alisema.

Kadhalika alisema uwanja huo utakapoanza kutumika utafungua fursa za kibiashara kwa wananchi wanaozunguka eneo hilo kwa kufanya biashara na huduma ndogo ndogo na muhimu kwa abiria.

Alisema uwanja huo utakuwa na maeneo ya kuegesha ndege, magari ya abiria, jengo la abiria, mnara wa kuangalia usalama wa ndege, mitaro ya kutoa na kuzuia maji kuingia ndani ya uwanja na uzio wake.

Mhandishi wa vifaa na ushauri wa Kampuni ya SMEC International L.t.d. Sosthenes Lweikiza alisema, mpaka sasa kilometa moja ya njia ya kuruka na kutua ndege imekamilika kati ya kilometa mbili wanazojenga na kuahidi kukamilisha ukarabati huo kwa wakati richa ya kuwepo kwa changamoto ya mvua za mara kwa mara.

Alisema, awali uwanja huo endapo ungekamilika ulitakiwa kutumiwa na ndege za aina ya ATR-72 lakini serikali imeongeza mita 200 za njia ya kuruka na kutua kwa ndege ili kuhakikisha ndege za ATCL- Bombadia Q4-100 zinatua uwanjani hapo na kwamba vifaa vinavyohitajika kama vile saruji na lami vipo na muda wowote njia hiyo itakamilika.

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Shinyanga(SPC), Greyson Kakuru alisema, serikali imekuwa ikifungua mtandao wa mawasiliano ya barabara na anga ili kurahisisha usafiri kwa wananchi wake, kuwashauri wananchi kuchangamkia fursa za kufanya ujasiriamali wakati uwanja ukapokamilika na kuanza kutoa huduma.

Ijumaa
Desemba 1,
2023

# Nipashe SIKU YA UKIMWI DUNIANI 2023



**Daktari aliyemtibu mgonjwa wa kwanza nchini afunguka mtihani wake na kilichomkuta kazini**

Ukurasa 12

# Ukimwi, Homa ya Ini na Ngono kutibiwa kwa mtindo dozi moja




Hafla mojawapo ya Siku ya Ukimwi Duniani, kama leo. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Yasmine Protace**

NI hatua mpya ya kuzinduliwa Mpango wa Kudhibiti Ukimwi, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini (NASHCoP), inayolenga kutokomeza maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi nchini, katika mfumo jumuishi.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasema mjini Dar es Salaam, kwamba licha ya mafanikio ya Mpango Taifa wa Kudhibiti Ukimwi, bado kuna changamoto ya maambukizi mapya.

"Tuna kazi ya kufanya hususani kupunguza na kutokomeza maambukizi mapya ya VVU kwa vijana wenye umri miaka 15 hadi 24, pia kutokomeza maambukizi mapya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

"Haiwezekani katika karne hii kwa kweli pamoja na wataalamu tulio nao, rasilimali, dawa tushindwe kuitokomeza hii hali," anatamka Waziri Ummy, akidokeza kuwapo ongezeko la maambukizi ya magonjwa ya ngono na homa ya ini nchini.

Pia, anasisitiza kwamba chombo NASHCoP, kwa kushirikiana na jamii kuendelea kuhimizana na kuhimiza makundi yaliyo hatari zaidi kama vile wasichana na wavulana katika rika balehe, kuzingatia huduma jumuishi.

Anashauri "wanawake na vijana, kinamama wajawazito na wanaonyonyesha pamoja na watoto wao kwenda kupata huduma jumuishi.

"Wataalamu wetu na jamii inayotuzunguka nao kufuatilia kutoa huduma hizo kwa weledi kulingana na miongozo inayotolewa na Wizara ya Afya."

Waziri Ummy anaendelea kutaja magonjwa yasiyoambukiza na anasisitiza jamii kuchukua tahadhari dhidi ya mtindo wao wa maisha na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

"Huu ndio ukweli, ukiwa na Ukimwi na ukazingatia dawa, unaishi vizuri kuliko ukiwa na sukari au presha ya damu. Tuogope magonjwa yasiyo ya kuambukiza na tuwe na tahadhari nayo," anasema.

Wadau wa afya katika mkutano huo, walielezwa hali ya maambukizi ya VVU kwa vijana wa umri miaka 15 hadi 24, yanatajwa bado yako juu, huku maambukizi yakiendelea kushika kasi kwa madereva wa magari masafa marefu, wavuvi na wanaofanya kazi za migodini.

"Bado tunakabiliwa na changamoto ya maambukizi kwa vijana wetu," anasema Waziri wa Afya, huku Mwenyekiti wa Jukwaa la Vijana Wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi Tanzania, Pudensiana Mbwiliza, anataja unyanyapaa ndicho chanzo kikubwa, wanashindwa kupima magonjwa ya ngono na Ukimwi.

Dk. Neema Mlole, Mratibu wa Huduma za Ukimwi katika Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe wizarani, anasema awali mifumo ilijikita kupima Ukimwi pekee, lakini sasa itaangalia upimaji wa magonjwa mengine ya ngono na homa ya ini.

Hata hivyo, Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Christine Musanhu, alisema huduma jumuishi si rahisi kama inavyoonekana na huenda likawa jambo gumu.

Waziri Ummy ana ufafanuzi kwamba, katika mwaka wa bajeti uliopo, 2023/24, katika robo ya kwanza na pili, viti 207 vilipelekwa kwenye halmashauri 160; vifaa tiba vya uchunguzi 82 wamepewa halmashauri 70, ndani yake zipo mashine aina ya OPG moja na CBCT moja, vyote vikiwa na thamani ya shilingi bilioni saba.

Pia, Waziri anasema, serikali imeongeza ufadhili kusomesha wataalamu sekta ya afya, hasa kwa nafasi za kibingwa na wabobezi ndani na nje ya nchi, kukitengwa shilingi bilioni nane, kuboresha huduma katika sekta ya afya.

**MABORESHO HUDUMA**

Waziri anaeleza serikali sasa, imeboresha huduma za afya kuanzia ngazi ya msingi hadi taifa, wakihakikisha wananchi wanapata huduma bora na za afya karibu kwenye maeneo yao

"Serikali kupitia Wizara ya Afya, wadau wa sekta na wataalamu wengine, tayari wamefanyia kazi hoja zote zilizoibuliwa na bunge na semina zimefanyika kwa makundi mbalimbali ndani ya jamii, kuhusu umuhimu wa bima za afya kwa wote," anatamka.

"Kwa sasa nchi yetu iko mbali katika utoaji wa huduma, kuna vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa magonjwa, huduma nyingi za kibingwa zinapatikana hapa hapa nchini.

"Pia, huduma za afya zimesogezwa sana kwa wananchi, hivyo kama serikali tuko tayari kutekeleza na kuhakikisha kuwa tunaendelea kuboresha huduma za afya kote nchini," anafafanua.

Asasi za kimataifa, shirika la WHO na Shirika la Misaada la Marekani - UNAIDS, yalihudhuria uzinduzi kuwa na wawakilishi wao, waliosifu juhudi za serikali inayoongozwa na Rais Dk Samia Suluhu Hassan, katika mapambano dhidi ya Ukimwi, wakiahidi wataendelea kuunga mkono juhudi hizo

# Daktari aliyemtibu mgonjwa wa kwanza nchini afunguka mtihani wake na kilichomkuta kazini

## • Simulizi; wenye VVU kujifungua, mabinti hatarini..


**Na Mwandishi Wetu**

SASA imetimu miaka 40 tangu kugundulika kwa ugonjwa wa Ukimwi nchini, ambao uliingia Afrika Mashariki mwaka 1983

Tabibu huyo anatajwa kwa jina la Callixte Twagirayezu, sasa akiwa na umri miaka 93, ambaye binafsi anakiri kilikuwa kipindi kigumu sana kwake, alichowahi kushuhudia maishani mwake.

Ansimulia kwamba akiwa kazini katika vipindi tofauti vilivyopishana siku kadhaa, akakabiliana na wagonjwa watatu tofauti, akishangaa wanaugua katika hali asiyoujua, lakini inafanana.

Hilo anasema hicho kikawa kitendawili kilchomuumiza sana kichwa, hata akachukua juhudi za ziada kwa mawasiliano ya wakati huo, akamuandikia barua rafikiye aliyekuwa wakati huo, katika nchi za Scandinavia wanabadilishane mawazo.



Dk. Callixte Twagirayezu, alitibu mgonjwa wa kwanza wa Ukimwi nchini. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Shughuli ndani ya Maabara ya Majaribio Chanjo ya Ukimwi.

Naye rafiki huyo akamjibu kwa kwa barua kinachoendelea duniani, akiambatanisha gazeti yenye makala inayofafanua kuhusu maradhi hayo mapya, Ukimwi. Huo ndio ukawa ndio mwanzo wake kuelewa, Dk. Twagirayezu, kwa wagonjwa walioko nchini.

Hapo nako anakiri akaiishi kazini kwa hofu kubwa namna ya kuwahudumia wagonjwa, hasa katika tahadhari ya maambukizi kwamba maradhio hayaponyeki.

Anaeleza namna kundi kubwa la Watanzania baadae wakaugua na kupoteza maisha katika kipindi kifupi, huku wao wanaotibu, pia wakiwa katika shaka kubwa kazini, ku9ingopo kuambukizsa.

Daktari huyo anataja eneo mojawapo la wajibu wake ni penye hatari ya kutrukiwa damu kutoka kwa kinamama wanaojifungua kwa njia ya operesheni, huku katika namna mbalimbali wagonjwa wanaugua na kupoteza maisha.

Hapo anafafanua, namna walivyowaopasua kwa haraka kutio amtoto na kumshona haraka asiathiriwe, maana vipimo wakati huo vya kumkagua mtu mwenye virusi au asiye nacho haikuwapo.

**MZIZI WAKE NCHINI**

Kuna tafsiri za kihistoria, maradhi Ukimwi kuanzia mkoani Kagera. Ni historia imeshasimuliwa mara kadhaa, ikiwamo kutoka kwa Rais Mstaafu wa Tanzania, Mzee Ali Hassan Mwinyi, ikifafanuliwa alipatikana eneo la Lukuyu.

Ni eneo kunakotajwa kuwapo mwingiliano wa kijamii, kutoka taifa jirani na nhasda madwereva wa malori wanavuka mipaka wakanyooshewa vidole kuchangia hali hiyo na umaarufu wake.

Kunatajwa kuwapo mashati yanayotamba zama hizo aina ya 'Juliana' yaliyovuyia umma kutoka nchin Jirani na waliopatiokan sana kwa madereva hao ni kinamama wa Lukuyui na maeneo Jirani.

Villevile kunma simulizi za mamlaka zenye historia rasmi za kitaalamu, zikitaja maradhi yaliazna duiniani mwaka 1981 na nchini kuingia 1983, mgonjwa wa kwanza kugundulika mkoani Kagera.

Kimsingi ni mkoa ulioathirijka sana na zama hizo ugonjwa ulipoingia walioumia zaidi wakiwa vijana

INAENDELEA UK. 14

DK. RADKA ARGIROVA

# MTAFITI ALIYEANZA KWA KUINGIZA VVU NCHINI MWAKE, UKAWA MTAJI KUTIBU RAIA MAMILIONI

**Na Mwandishi Wetu**

MNAMO mwaka 1985, katika kilele cha Vita Baridi dunia ilikabiliwa sana na wimbi la maambukizo na vifo vilivyosababishwa na virusi vipya vya kushangaza.

Ugonjwa wa Ukosefu wa Kinga Mwilini, kwa kifupi 'UKIMWI', ulikuwa umetambuliwa kuwa ugonjwa mpya mwaka 1981. Kukawapo idadi kubwa inayoongezeka, vifo vya wapenzi wa jinsia moja, hata kutokana na maambukizi hayo yasiyo ya kawaida na adimu.

Ulijulikana pia kuwaathiri watumiaji dawa za kulevya kwa kujichoma sindano, huku ripoti ikifafanua:"Ni hali ambayo huwaweka wagonjwa kwenye maambukizo ya magonjwa mbalimbali. Ukimwi unaonekana kumaliza kinga ya wagonjwa na mara nyingi huwa hatari kwa sababu hiyo."

Miaka kadhaa baadaye, virusi vya Ukimwi (VVU) vilitambuliwa kuwa chanzo chake. Watu waliogopa na kampeni kuhusu ugonjwa huo zilizinduliwa katika nchi nyingi.

Hata hivyo, katika nchi kama Bulgaria, ambayo ilikuwa na siasa za Kikomunisti, pia mfumo hodhi wa ndani, yenyewe ilikataa kukiri tishio hilo, wakielezea kama 'ugonjwa wa wapenzi wa jinsia moja', wakimaanisha tatizo lililotawala kwa nchi za Magharibi pekee, licha ya ukweli wanafunzi wa kigeni na mabaharia walikuwa wakifa katika hospitali za Bulgaria.

**MTAALAMU AFUNGUKA**

Dk. Radka Argirova, mmoja wa wataalamu wa kwanza wa virusi nchini, alifanya kazi katika taasisi ya utafiti jijini Sofia, Bulgaria.


"Nilikuwa nikifanya kazi katika moja ya maabara ya Chuo cha Sayansi cha Bulgaria na kulikuwa na maabara ya kuvutia sana ya magonjwa ya virusi katika taasisi hiyo," Argirova amasema.

Moja ya virusi vya binadamu ambavyo yeye na wenzake walikuwa wakichunguza ni VVU, lakini wakati virusi hivyo vilikuwa vinajulikana, 'ugonjwa mbaya' chanzo chake hakikujulikana.

Haikuwa rahisi kwake kuondoka Bulgaria, lakini mnamo Juni 1985, Daktari Argirova, akapata fursa akasafiri kwa ndege hadi Hamburg, nchini Ujerumani Magharibi wakati huo, kuhudhuria mkutano wa kisayansi ili kuwasilisha matokeo ya utafiti wake.

Hapo ikaendana na katika siku hizo, nchi chache katika miaka ya 1980, zikianzisha kampeni za kuudhibiti ugonjwa Ukimwi.

Unatajwa kuwa mkutano wa kuvutia kitaalamu. Madaktari kadhaa wakubwa wanaovijua virusi duniani walihudhuria, akiwamo mtafiti mashuhuri wa Marekani Dk. Robert Gallo.



DK. RADKA ARGIROVA

"Hatukuwahi kufikiria kwamba ingeenea haraka hivyo kwa sababu aina hii ya virusi ni vigumu kusambaa, lakini polepole inaenea katika maeneo mbalimbali ya dunia," Dk. Gallo akatamka.

"Hatukuwahi kutarajia kiwango cha juu cha vifo kutokana na virusi hivi. Asilimia ya watu walioambukizwa ambao huwa wagonjwa sana ni kubwa na inaongezeka (wakati huo mwanzoni mwa miaka ya 1980)."

Hapo ndipo Dk. Gallo akaanza kuteta jambo na swahiba kwenye fani, mwenzake, Dk. Argirova.

"Wakati huo nilikuwa nikivuta sigara na akanijia kuniomba sigara. Alipojua nilikotoka, aliniuliza: 'hali ya Ukimwi ikoje huko Bulgaria?" anasimulia Dk. Gallo, akikumbusha alivyojibu swali hilo:

"...nilijibu 'siwezi kukuambia', kwa sababu hatuna uchunguzi, kwa hiyo sijui chochote kuhusu hilo. Tunahitaji kufanya vipimo."

Dk. Gallo anasimulia kilichojiri "alisema, 'tafadhali fanyeni' nami nikajibu 'ndiyo, lakini sina virusi (hakuna wanaougua)."

Hapo akapata suluhisho, akimwomba Mjerumani mwenzake kuandaa VVU katika maabara yake na kuifunga kwenye bakuli lenye ukubwa wa simu ya mkononi ya kisasa.

Siku kadhaa baadaye ni kwamba, walimpa Argirova ili ampelekee Sofia kwenye begi lake, hapo mtaalamu wa virusi akitolea ufafanuzi: "Ilikuwa nyekundu na hukuweza kuona virusi au seli.

"Ilikuwa kama divai nyekundu na ilikuwa na bakuli mbili, moja ikiwa na seli zilizoambukizwa na nyingine ikiwa na seli ambazo hazijaambukizwa."

"Nilichukua chupa ndogo, nikaziweka kwenye begi langu na kusafiri hadi Frankfurt," anaeleza Dk. Gallo.

Marafiki hao wakakutana kwenye uwanja wa ndege na pamoja wakarudi kwenye maabara katika Chuo cha Sayansi cha Bulgaria, ili kuhifadhi virusi kwa nyuzi joto 37.

Dk Gallo ana simulizi kwamba, hakuwa na uhakika wa chembechembe hizo za VVU kama zilibaki salama kwa safari yake, akinena:

"Seli na virusi huteseka kidogo wakati haviko nyuzi 37 na safari ilikuwa ya mshtuko kwao, kwa hivyo walilazimika kwenda kwenye 'incubator'. "Lakini Jumatatu (siku iliyofuata), nilifurahi kuona jinsi seli zilivyoonekana vizuri na nikaanza kukusanya nyenzo."

Wakati seli za VVU zilianza kustawi katika nyumba yao mpya, kwa mwenyeji Dk. Argirova mambo yakazidi kuwa mabaya, simulizi dhidi yake zikienea kwamba, ameleta virusi hivyo hatari nchini, hata wanasayansi wenzake waliogopa.

"Kulikuwa na kelele nyingi kwenye magazeti na kulikuwa na watu ambao hawakufurahishwa...wengine waliogopa sijui kwanini na wengine, labda na wivu kidogo," anasimulia Dk. Argirova

**UCHUNGUZI WAIVA**

Dk. Argirova akaonekana kwenye rada ya huduma za usalama serikalini, hata akatakiwa kujieleza kwa kina safari ya virusi hivyo nchini kwake, Bulgaria na vilivyotoweka.

Anasimulia: "Watu kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani (wana Usalama) walianza kuniuliza kila siku kuhusu jinsi Gallo alinipa virusi, kwanini, nia yake ilikuwa nini...Maswali ya aina hiyo kila siku, kila siku, kila siku! Nimechoka kueleza!"

Licha ya upinzani wote wa awali, Dk. Argirova akapata washirika waliomuunga mkono kutoka mamlaka ya Kikomunisti na hatimaye, akapata kibali cha kuwakusanya wenzake na mfumo wa kufanya majaribio ya kuikabili. Mnamo mwaka 1986, vituo 28 vya majaribio viliwekwa nchini kote Bulgaria na wananchi milioni mbili walipimwa kama wanavyo VVU.

Katika filamu iliyoandikwa miaka mitatu baadaye, msimulizi anasema kwamba redio, televisheni na vyombo vya habari viliripoti kila mara kuhusu tatizo la Ukimwi.

INAENDELEA UK. 14



TAFAKURI YA MLALAHOI

# Viongozi wetu jueni sote tuna haki sawa




KUNA wakati mimi hukaa na kufikiria kauli nzito iliyopata kutolewa 'kama ya Tanzania yanakushinda, basi bora ukahamia nchi jirani..."

Naendelea kufikiria, naona kama alikuwa akifanya utabiri fulani hivi wa maisha yanavyoendelea nchini, unaona kabisa uhusiano baina ya wananchi na watu wanaowategemea kuwaonyesha njia ya kimaisha unadorora.

Unaona kabisa kiongozi mwenye dhamana ya kuongoza wananchi, anakiuka dhamana hiyo na kuvamia dukani kwa mwananchi wake na kumlazimisha ampe kitu anachotaka ikiwa ni pamoja na fedha.

Kiongozi anajiamulia kuchukua hatua mkononi kwa kufyeka watu masikio na vidole huku wengine akiwadunga bisibisi za mgongo na kuwaachia kilema cha maisha na yeye akiendelewa kutamba uraiani akidai ni maagizo kutoka juu!

Mwananchi analalamika mpaka vyombo vya sheria, mhusika anawekwa mbaroni na anafunguliwa kesi, anashindwa na kufungwa, lakini anakata rufani na kuchomoka kifungoni, huku mwathirika wa vitendo hivyo akiangalia.

Kigogo huyo mhusika anaulizwa kwanini kufanya vile, anakwambia aulizwe wa juu yake aliyempa dhamana ya kusimamia eneo fulani la ndani ya nchi! Unabaki unashangaa na kufikiria njia ya kuingilia jirani.

Mwingine anajulikana kabisa kuna shauri dhidi yake mahakamani, lakini kana kwamba haijulikani, anapewa dhamana ya kuongoza wakati awali ilishamshinda mpaka kufunguliwa kesi mahakamani.



**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

Unajitazama unaona afadhali uwe mbali na uliko kwa kweli.

Leo tunasikia kijana kafanyiwa ya kufanyiwa na kiongozi mzito tu wa serikali, ambaye badala ya kulinda maisha ya kijana huyo, ndiyo kwanza anamdhalilisha!

Anasingiziwa mengi eti kaenda kuroga na simulizi nyingi kuhusu teknolojia hiyo, akachezeshe kwa sangoma, ili biashara sijui ikose wateja au kitu gani vile!

Fikiria kijana analalamika anawekwa ndani na polisi kwa siku kadhaa, tena baada ya kutishiwa na mheshimiwa tajiri.

Kigogo wa polisi anaulizwa na wanahabari kuhusu tukio hilo, anajibu harakaharaka eti hajui lolote kwani yuko msibani! Tukio la aina hiyo linatokea eneo lako la kazi unasema uko msibani kweli? Usalama wa raia uko wapi?

Bosi wa mkoa anayewakilisha dola katika eneo hilo, naye anaulizwa anasema hana taarifa yoyote kuhusu hayo kudhalilishwa na mwakilishi wake Kweli? Hizo taarifa zingine anazowasilisha kwa bosi wake huzitoa wapi?Tukio kama hili la kutishia maisha ya mtu lakini pia la kumdhuru na kumdhalilisha kiasi hiki linatokea mkoani, Polisi haijui eti iko msibani na mkoa haujui eti haujapata taarifa, kweli? Kwenda jirani kunazidi kutuita ati!

Ni kawaida ya Watanzania unapokuwa huna madaraka, utanyenyekea kwa Wananchi, lakini ukishayapata basi utajitwisha madaraka yanayomkaribia Mungu na kuona wananchi waliokuweka hapo si kitu tena kwako.

Viongozi wengi wanaofanya madudu kama hayo, wanapokuwa wameondolewa kwa kutenguliwa uteuzi au kutumbuliwa au hata kumaliza muda wao wa majukumu, hujigeuza ili kuonekana rahim kinafiki.

Angalia sasa mheshimiwa huyu aliyeamuru watu kumdhalilisha kwa satili ya madhara, leo mtendaji mamlaka kumgeukia, ataonekana kunyenyekea na kujishusha ili kujifanya yuko karibu na wananchi wake. Nini hii!

Nafikiria mathalan leo tungeambiwa mzito huyo amefanyiwa hayo na wananchi, hivi hao wananchi wangetokaje?

Au Kamanda kafanyiwa hivyo na wananchi achilia mbali kafanyiwa sijui nani mzito zaidi, hao wananchi wangekuwa wapi?

Lakini kwa kuwa ni masikini kafanyiwa hivyo, basi ni haki yake kwa sababu aliyefanya ni bosi serikalini, basi wana usalama hawajui au watasuasua kumnasa mhusika, na wengine wa juu hawajui kulikoni, kwa kuwa masikini na wanawe, tajiri na mali zake.

Wale jamaa zetu wa hakijinai bila shaka hata hii tabia waliiona na kwenye taarifa yao wakaiweka, lakini mambo bado ni yale yale, kina kijana yule, pangu pakavu tia mchuzi, wanazidi kukalia hilo, kwani hawana haki mbele ya wakubwa wenye nacho.

Kwanini binadamu tunapoteza huruma, utu na ubinadamu wetu kwa sababu ya nafasi tulizonazo? Hivi wananchi nao wakitaka unyonge wao kujitetea dhidi ya viongozi wao, nchi hii itakalika kweli? Viongozi hamkupewa nafasi hizo kutumia mabavu kujitwalia haki zisizo zenu au kudhalilisha, kuumiza na kuua watu!

Tumpongeze Chifu Hangaya kwa kulipata hili na kuchukua hatua sawia na kutengua uteuzi ili kupisha uchunguzi, wahusika wafikishwe mbele ya vyombo vya sheria na haki hatimaye ionekane imetendeka.

**Mungu Ibariki Tanzania.**

## SIKU YA UKIMWI DUNIANI, 2023

# Daktari aliyemtibu mgonjwa wa kwanza nchini afunguka mtihani wake na kilichomkuta kazini




Hospitali ya Ndolage, wilayani Bukoba, Kagera, walikotibiwa wagonjwa wa kwanza wa ukimwi nchini, 1983. **PICHA: MTANDAO**

**INATOKA UK.12**

na hadi miaka mitatu badaaye, ulishaenea sehemu nyingi za nchi.

**HALI ILIVYO LEO**

Hadi sasa duniani, Tanzania inatajwa katika orodha ya nchi tano enye mwelekeo wa kutokomeza Ukimwi ifikapo mwaka 2030, kuendana na program ya kidunia, chini ya usimamizi wa Umoja wa Mataifa.

Eneo la Kusini mwa Jangwa la Sahara, ambako Taznania inapatikana, kunatajwa asilimia 65 ya watu wote wenye VVU wanaishi, pia kuna hatua kubwa inapigwa katika kutokomeza ugonjwa huo.

Ndani ya orodha hiyo, kuna nchi za Botswana, Eswatini, Zimbabwe na majirani Rwanda na Tanzania, zikiwa katika kile kinachoitwa '95-95-95', kwa mujibu wa Shirika la Umloja w Mataifa Kupambana an Ukimwi (UNAIDS).

Hapo maana yake ni kwamba, katika kundi la watu asilimia 95ya wanaoishi na VVU wanajua hali zao na wanapata matibabu ya kurefusha maisha. Pia, ndani ya kundi hilo, asilimia 95 yawanaopata matibabu, wamefanikia kufubaza virusi hivyo, hata haiwezekani kwao kusambaza.

Inatajwa kwamba kuna mataifa mengine 16 duniani, kato yao nane yako barani Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara yanakaribia kufikia lengo hili.

"Mwisho wa Ukimwi ni fursa ya urithi wenye nguvu ya kipekee kwa viongozi wa leo," Winnie Byanyima, Mkurugenzi Mtendaji wa UNAIDS, anatamka katika taarifa yake, akiongeza:

"Wanaweza kuokoa mamilioni ya maisha na kulinda afya ya kila mtu. Wanaweza kuonyesha kile ambacho uongozi unaweza kufanya."

"Ukweli na takwimu zilizoshirikiwa katika ripoti hii hazioneshi kuwa kama ulimwengu tayari tuko njiani, zinaonyesha kuwa tunaweza kuwa," anafafanua Byanyima.

**WASICHANA HATARINI**

Kunatajwa wanawake na wasichana wa rika zote walichangia asilimia 63 ya maambukizi mapya ya VVU mwaka jana.

Jaribio la chanjo ya VVU linaendelea nchini Uganda, Tanzania na Afrika Kusini, likichanganya chanjo za majaribio za VVU na mengine (pre-exposure prophylaxis -PrEP) kwa wakati mmoja, jambo ambalo halijawahi kufanywa hapo awali.

Nchini Botswana, nako wasichana wanatajwa kusalia katika hatari, huku wanaume wazee wanawawinda katika dhana inayoitwa 'ngono kati ya vizazi'.

Katika hilo, mawanamke Gaone mwenye umri wa miaka 32, anasimulia alivyoambukizwa VVU akiwa msichana shule, akitamka alichangiwa na ndugu yake wa karibu walihusiana vizuri, ndipo akamuingiza kwenye ulingo wa mapenzi.

Gaone amekuwa akitumia dawa za kurefusha maisha tangu mwaka 2012, sasa akiwa mama wa watoto wawili, wasio na VVU, akityuimia katika kampeni kuikabili kuasmbaa Ukimwi, ambayo sasda inawezekana hata kwe walioambukizwa, kujifungua na kuonyoyesha watoto kwa miezi mingi

Anaeleza uzoefu wake, ni kwamba, jamii haiko tayari kuzungumza wazi kuhusu uharamia wa kingoni kati yao. Hapo anatyoa Ushahidi akiwa mwanaharakati kuwa:

"Katika baadhi ya siku, ninapokea jumbe kutoka kwa wanawake wengi kama watano waliopata VVU kutoka kwa wazee, wengi wao wakiwa jamaa zao. Ikiwa wanaume hawatasikiliza, tunaweza kufanya nini?"

**DALILI ZAKE**

Dalili za kawaida zinazofanana na dalili za maambukizi mengine ya virusi, kama vile homa ya mafua na huweza kujumuisha:

- Homa
- Uchovu
- Tezi za limfu kuvimba
- Koo kuuma
- Maumivu ya kichwa na misuli kuuma

**Dalili nyingine ni pamoja na:**

- Upele mwekundu
- Kutokwa jasho usiku
- Kupoteza hamu ya kula
- kupungua uzito

**MZIZI KWA HATUA**

Anakumbuka mnamo mwaka 1983, katika Hospitali ya Ndolage, alikokuwa anatumikia, Dk. Twagirayezu akiwa Mganga Mfawidhi, akapata wagonjwa watatu, wanaume wawili na binti mmoja.

"Mwanaume alikuwa na ishara ya kifua kikuu. Hata hivyo vipimo vikakataa. Mwingine akawa kama na magonjwa ya kuambukizwa kingono....

"Binti akawa anaharisha, lakini tukashindwa kugundua ilikua ana ugonjwa gani vile," anakumbuka mtihani wake mkuu wa kitaaluma, hata akawa na wenzake wakachanganyikiwa, ni aina gani hiyo nchini Tanzania.

Hata hivyo, ilikuwa miaka miwili baada ya Marekani kuripoti kuwapo kirusi kipya kwao "Ugonjwa wa Upungufu wa Kinga Mwilini.'

Mtaalamu huyo anaeleza kutajwa kuwapata mashoga watano huko, ingawaje katika umbali wa Tanzania, ilionekana kama haitafika na ni jambo la huko ughaibuni.

Hapo kwa wagonjwa wao watatu wapya, wakabaki wanaumiza akili madaktari 'nini hicho?' Hapo ndipo Dk. Twagirayezu akamkumbuka rafikiye raia wa Sweden, akaamua kumuandikia barua ya kirafiki na yule hakukawia kumjibu haraka, akimuambatanishia jarida liitwalo Lancet na ukurasa wa kusoma, ikimpatia majibu ya swali lake.

Ni miezi michache baadaye kukatangazwa duniani, ni maradhi yatokanayo na virusi vikiathiri damu ya binadamu.

Elimu hiyo ikamfanya Dk. Twagirayezu, arudi haraka kwa mgonjwa wake, yule binti akimhoji kama ana mpenzi au kaolewa.

Anasimulia mgonjwa akamjibu ana mpenzi anayeishi eneo la Nshamba (Bukoba) na akapata wa urafiki wa miaka saba. Wakati binti huyo anaendelea kutibiwa, na daktari huyo, akafariki.

Dk. Twagirayezu, anasimulia tangu hapo namna alivyomfuatilia mgonjwa wa Ukimwi aliyemjua tangu mwaka 1985, ambaye mkewe alifariki kipindi hicho, lakini mume huyo yuko Bukoba mjini hadi sasa anaishi.

Pia licha ya uzee wake sasa ni mstaafu, anasema bado anafuatilia mno maradhi ya virusi, ikiwamo Covid 19.

**ULIVYOGONGA HODI**

Hakuna taarifa sahihi sana, namna ulivyoingia nchini, ila inaaminika imetokea nchi jirani Uganda, mpakani katika kijiji cha Rukunyu, Wilaya ya Misenyi, kulikokuwapo 'soko pori' la bidhaa mahali hapo, wakati huo kulikuwa na uhaba wa baadhi ya bidhaa nchini.

"Watu walikuwa wanakutana sana katika eneo hili," anakumbuka Dk. Twagirayezu. "Watu waliumia sana kuugua, upande wa pili Uganda, wakasema wenzao wa upande wa pili (Tanzania) wamewaroga, kwa sababu ya biashara zao ziko juu".

- **Jarida hili la siku maalum na makala zake, limeandaliwa na Peter Orwa.**

# MTAFITI ALIYEANZA KWA KUINGIZA VVU NCHINI MWAKE, UKAWA MTAJI KUTIBU RAIA MAMILIONI

**INATOKA UK.12**

VVU hatimaye vikawa hadharani na Dk. Argirova na wenzake wakaweza kumchunguza kwa uhuru aliyeathiriwa na jinsi vilivyombukizwa.

Miaka minne baada ya kuingiza virusi hivyo nchini mwake kwenye begi lake, Dk. Argirova akapewa jukumu la kuelimisha umma wa Bulgaria kuhusu VVU na Ukimwi, na vita vya kuvidhibiti.

Miaka mingi imepita sasa, wastani wa miaka 37, mkongwe huyo hadi mwanzoni mwa mwaka huu amebobea, katika daktari mtaalamu wa virusi katika moja ya hospitali kubwa binafsi nchini Bulgaria, pia ni gwiji kitaifa kwenye harakati za kukabili maradhi mapya ya Covid 19 nchini mwake.



# Mwongozo kusimamia huduma za afya nchini mbioni kukamilika

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema ipo hatua za mwisho kukamilisha mwongozo utakaosimamia utoaji huduma za maabara nchini ili kukomesha tabia ya baadhi ya wataalam kutoa majibu ya uongo kwa wagonjwa hali inayohatarisha afya za wananchi.

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Uchunguzi Wizara ya Afya, Gerald Mrema, alibainisha hayo juzi jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye hafla ya kufunga mafunzo ya viongozi chipukizi wa huduma za maabara nchini.

Alisema serikali imekuwa ikisikia malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi ya kupatiwa majibu yasiyo sahihi kutoka kwa wataalam wa huduma za maabara nchini.

"Ili kukabiliana na hali hiyo serikali ipo katika hatua za mwisho kukamilisha mwogozo ambao utatumika kusimamia utoaji wa huduma za maabara nchini ili kuwabana wote ambao wamekuwa wakitoa majibu feki ya vipimo lakini pia utamwezesha mwananchi kujua hatua gani achukue ili kupata huduma sahihi,"alisema.

Akizungumzia mafunzo hayo alisema lengo ni kuboresha utoaji huduma za maabara nchini, ambao unachangizwa kwa kiasi kikubwa na uwekezaji uliofanywa na serikali katika sekta ya afya nchini.

"Mafunzo haya yanalenga kuboresha utoaji wa huduma za maabara nchini hii yote ni kutokana na serikali kuwekeza kwa kiasi kikubwa kwenye sekta ya afya kwa kujenga vituo vya afya, zahanati pamoja na hospitali hivyo lazima tuboreshe pia utoaji wa huduma za maabara ili wananchi wapate huduma sahihi,"alisema.

Awali, Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dk. Elius Kwesi, alisema kada ya wataalam wa afya ni eneo nyeti katika utoaji wa huduma za afya nchini.

Alisema, kutokana na hali hiyo eneo hilo linapaswa kuimarishwa ili huduma zitakazotolewa ziwe bora na wananchi wapate dawa kulinga na kile wanachoumwa na siyo vinginevyo.

"Maabara ndiyo eneo muhimu katika utoaji wa huduma za afya, bila vipimo huwezi kutoa dawa hivyo ipo haja ya kuhakikisha eneo hili linawekewa mkazo zaidi na fedha ambazo zinaletwa na wahisani lazima tujitahidi kuwekeza kwenye kuboresha huduma za maabara nchini"alisisitiza

Mmoja wa wahitimu wa mafunzo hayo mtaalam wa maabara kutoka hospitali ya Rufani ya mkoa wa Arusha (Mount Meru) Philipo Mathias, alisema mafunzo hayo yatasaidia kuboresha utoaji wa huduma za maabara nchini.

"Mafunzo haya yatakuwa msaada mkubwa sana kwetu kwani moja ya changamoto ni wataalam kutozingatia taratibu za ufanyaji vipimo lakini pia kuhakiki ubora wa vifaa vyetu kabla ya kuvitumia hali ambayo imekuwa kisababisha wakati mwingine kutoa vipimo visivyo na uhakika kwa wananchi,"alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Halima Bulembo (wa nne kulia), akipokea sehemu ya msaada wa viti na meza kutoka kwa Kaimu Meneja wa Benki ya CRDB Kanda ya Dar es Salaam, Muhumiliza Buberwa vilivyotolewa na benki hiyo jana, kwa ajili ya Shule ya Sekondari Lingato ya wilayani humo. Wengine ni Meneja wa Benki ya CRDB Kanda ya Pwani, Badru Idd (wa pili kushoto), Meneja wa Benki hiyo, Tawi la Kibada, Isaya Lyimo, Meneja Mwandamizi Idara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Benki hiyo, Suzan Shuma (wa tatu kushoto), Kaimu Ofisa Elimu Sekondari wilaya hiyo, Emmanuel Mwakalinga (kulia), Kaimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Kisarawe II, Ashura Bihongo na Kaimu Katibu Tawala Wilaya hiyo, Adellah Ntenjera. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# RC: Wataalam wasaidieni wakulima

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa mkoa wa Dodoma Rosemary Senyamule, amezindua rasmi msimu wa kilimo 2023/2024 na kuwataka wataalamu wa kilimo kuwasaidia wakulima kulima kwa tija ili kukuza uchumi wa taifa na mtu mmoja mmoja.

Uzinduzi huo ulifanyika juzi katika viwanja vya shule ya Sekondari Mazae, Wilaya ya Mpwapwa Mkoani Dodoma.

Senyamule alisema malengo ya msimu huu wa kilimo ni kila kaya na taasisi kama shule kulima angalau heka mbili za mtama.

Alitaja mazao mengine ya chakula yanayopewa kipaumbele kuwa ni uwele, mpunga , muhogo, viazi vitamu, maharage, kunde, mbaazi, njegere, choroko, viazi mviringo na mahindi ambapo matarajio ni kulima tani 170,235.

Alisema mazao ya biashara ambayo yatalimwa katika msimu huu wa kilimo ni pamoja na alizeti, korosho, karanga na ufuta kiaso cha tani 13,350.

"Rais ameendelea kuimarisha njia sahihi na kuonyesha kilimo ni uti wa mgongo kwani katika kipindi cha miaka mitano, amewekeza nguvu nyingi katika uchumi wa viwanda ikiwemo shughuli za umwagiliaji na mkoa wetu tukiwa wanufaika wakubwa. Alisema Rais Samia pia ametoa ajira kwa maofisa kilimo kwa kuwapatia vitendea kazi na kuwapatia vifaa vya kupimia udongo ili wakulima walime kulingana na mazingira na kuendeza uchumi wa kilimo, " alisema Senyamule.

Kadhalika, alitoa wito kwa maofisa kilimo kutoa hamasa ya kutosha katika vijiji kwa kufanya shughuli za kilimo kuwapimia udongo wananchi ili kuwasaidia kujua aina ya mazao ya kulima kwenye mazingira yao.

Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Ally Gugu, alitoa wito kwa wakulima wote wa mkoa na taifa kuzingatia elimu wanayopewa na wataalamu wa kilimo ili kuongeza uzalishaji na kuifaharisha Dodoma katika sekta ya kilimo.

Aliwaagiza wananchi kushiriki kikamilifu kwenye msimu huu wa kilimo ili kuwa sehemu ya kulima mazao ya chakula na si kulia njaa na kutaka msaada kutoka serikalini.

# Dodoma jiji kinara mbio za Mwenge

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imeibuka kuwa kinara katika mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2023 baada ya kushika nafasi ya kwanza kimkoa, kikanda na nafasi ya pili kitaifa.

Mkuu wa mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema hayo alipokuwa akitoa maelezo mafupi kuhusu matokeo ya mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2023.

Akizungumza na wakuu wa wilaya na watendaji, Senyamule alisema kwa mwaka 2023 Mkoa wa Dodoma ulikuwa wa 30 kabla ya kukimbiza Mwenge wa Uhuru.

"Ushindi huu niwaambie wakimbiza Mwenge wa Uhuru wanakuwa na vigezo ambavyo wanavyoangalia kama vile kwenye upande wa fedha zilizoletwa zimetumikaje, ubora wa miradi imesimamiwaje kwa tija na ufanisi kiasi gani,walivyohamasishwa wananchi kupokea ujumbe wa Mwenge wa Uhuru wa kitaifa" alisema Senyamule.

Mkuu huyo wa mkoa alisema kuwa alipokea barua kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Vijana, Kazi na Watu wenye Ulemavu ikionesha matokeo ya Mwenge wa Uhuru mwaka 2023 kwa kila halmashauri, kimkoa, kikanda na kitaifa.

Alisema halmashauri tano zimeingia kwenye kumi bora,kati ya hizo Jiji la Dodoma limeshika nafasi ya kwanza kimkoa, kikanda na nafasi ya pili kitaifa.

Alisema halmashauri nyingine zilizoingia 10 bora ni ya Mji Kondoa ambayo imeshika nafasi ya pili kimkoa, kikanda na nafasi ya sita kitaifa, huku Wilaya ya Mpwapwa ikipewa ya tatu kimkoa, kikanda na nafasi ya nane kitaifa.

Senyamule alizitaja halmashauri nyingine zilizopo ndani ya mkoa huo kuwa ni ya Wilaya ya Kondoa na Kongwa ambazo zilifungana kwenye nafasi ya nne kimkoa, nafasi ya nne kikanda na nafasi ya 10 kitaifa.

"Matokeo hayo yamepelekea mkoa wa Dodoma kufikia asilimia 83.54 ya ufanisi kwenye shughuli za Mwenge wa Uhuru mwaka 2023, ambapo kwa mwaka 2022 tulishika nafasi ya 22 kitaifa jambo hilo halikutufurahisha,"alisema.

Alisema kutokana na matokeo hayo na juhudi mbalimbali zilizofanyika mwaka huu kwa mara ya kwanza katika historia ya mkoa wa Dodoma wameshika nafasi ya kwanza kitaifa.





# Ziwa Nyasa latajwa chanzo kukuza utalii

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

FUKWE za Ziwa Nyasa katika wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya, zimetajwa kuwa miongoni mwa maeneo yenye vivutio vya watalii nchini ambavyo vikitangazwa vizuri vinaweza kuongeza idadi ya watalii na kulipatia taifa fedha za kigeni.

Ofisa Utalii wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Noah Mbopoma, aliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya maofisa wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yenye vivutio hivyo.

Ziara ya maofisa hao ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Kukuza na Kuendeleza Utalii Kusini (REGROW) ambao unalenga kukuza utalii wa vivutio mbalimbali vikiwemo utalii wa utamaduni na vitu mbalimbali vya asili.

Mbopoma alisema katika ufukwe wa Matema kuna pango ambalo liliwahi kutumiwa na wapiganaji wa Vita vya Pili vya Dunia mwaka 1939-1945 kujificha ili kuwakwepa maadui.

Alisema pango hilo kwa sasa ni kivutio kizuri cha utalii kwa watu wengi kwenda kuangalia na kujifunza mambo ambayo hayapatikani sehemu zingine.

"Lakini pia kwenye ufukwe huu kuna samaki wa rangi ambao hawapatikani sehemu nyingine nchini ambao wanatumika kwa ajili ya mapambo kutokana na rangi zao kuvutia," alisema Mbopoma.

Alisema ufukwe huo pia una mchanga ambao hauna tope wala vumbi na hivyo unawavutia watu wengi kufurahia utalii wa boti ndani ya ziwa hilo.

Alitaja changamoto zilizopo kwenye ufukwe huo ni kutokuwepo kwa hamasa ya kutosha na utaratibu mzuri wa waongoza watalii wa eneo hilo jambo linalosababisha serikali kupoteza mapato. Ofisa Uhusiano wa TTB, Augustinah Makoye, alisema ufukwe huo ni miongoni mwa maeneo ambayo mradi wa REGROW unatekelezwa kwa kutoa elimu kwa wananchi kutambua fursa zilizopo na kuzitumia.

Alisema ufukwe huo wa Matema uko pembezoni mwa safu za Milima ya Livingstone na hivyo watalii wanaweza wakafurahia ubora wa fukwe na muonekano wa milima hiyo.

Mmoja wa vijana wanaofanya kazi ya uvuvi kwenye eneo hilo, Amani Mwandosya, alisema wageni wanaotembelea eneo hilo wamekuwa wakiwaachia vitu mbalimbali ambavyo vinawafaidisha.

Alisema utalii pia unawanufaisha wakazi wa eneo hilo kwa kuwa wamekuwa wakiuza bidhaa mbalimbali za utamaduni ikiwemo vyungu na kujiongezea kipato na kuomba serikali kuboresha zaidi mazingira ya eneo hilo ili kuongeza idadi ya wageni.

"Hapa huwa wanakuja hata wazungu ambao wanakuja kufurahia hapa hali nzuri ya hewa na kujifunza mambo mbalimbali, hapa sasa hivi baadhi ya watu wanajenga hoteli za kisasa kwa sababu ya wageni hao ambao huwa wanakuja," alisema Mwandosya.

Agosti, mwaka huu, wakati wa Maonyesho ya Wakulima (Nanenane) yaliyofanyika kitaifa mkoani Mbeya, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa aliliagiza Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kuwekeza kwenye kutangaza vivutio vilivyoko kusini mwa Tanzania ili kuwapo na msawazo wa utalii kati ya eneo hilo na Kaskazini.




Mkurugenzi wa taasisi ya Victorious Centre of Excellence, Sarah Laiser (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu ujio wa mkutano wa kimataifa unaolenga kujadili changamoto zinazohusiana na usonji na utindio wa ubongo ulioandaliwa na taasisi hiyo kwa ushirikiano na Autism Connect unaotarajiwa kufanyika Desemba 2 hadi 3 mwaka huu katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) katika jiji hilo. Kushoto ni Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa taasisi ya Autism Connect, Dolly Thakkar na Mtaalamu wa Masuala ya Afya, Dk. Issack Maro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Watoto mitaani bado changamoto

**Na Elizabeth John,** NJOMBE.

OFISA Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Mji Njombe, Vikiana Kihwelo, amewaomba wadau wa maendeleo kuwapa msaada wa kielimu watoto wanaozurura mitaani ili kuwaondoa katika mazingira hatarishi.

Alisema watoto 314 kati ya 22,958 katika halmashauri hiyo wanaishi katika mazingira magumu ya kujilea peke yao hali ambayo inasababisha kukosa elimu pamoja kujitafutia chakula na mahitaji mengine.

Alisema baadhi ya watoto hao wanaishia mitaani kwa kukosa ndugu au walezi wa kuwaangalia hali inayowalazimu kukatisha masomo ili wajilee. Kihwelo.

"Kuna watoto wapo wanazurura kwenye soko letu wanaomba omba hao wote tunahitaji kuwasaidia,aidha wapelekwa shule,vyuo vya ufundi ili waweze kujiendeleza.

Katibu tawala wilaya ya Njombe, Aghata Mhaiki aliwataka wadau kuungana ili kusaidia watoto hao kuepukana na matukio ya ukatili wa kijinsia.

Aliwasihi wanapomuona mtoto anapata shida wachukue jukumu la mzazi na kumsaidia kwa kuwa mkoa huo una matukio mengi ya ukatili wa kijinsia kama vile ubakaji, unyanyasaji, kutenga watoto ila sisi kama wadau sisi wadau,sisi kama wazazi ni jukumu letu kuwasaidia,

Meneja wa Mradi wa Kizazi Hodari Kanda ya Kusini kutoka taasisi ya Diloite, Revocatus Kashaga, alisema jamii inalojukumu ya kusaidia watoto hao ili ku-

# Serikali yasisitiza usafi kuepuka kipindupindu

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya, katika Mkoa wa Mbeya, imewasisitiza wananchi kuzingatia usafi wa mazingira kwenye maeneo yao ya biashara na kwenye makazi ili kuepuka magonjwa ya mlipuko kikiwemo kipindupindu.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Simon Mayeka, alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na wananchi wa kata ya Ifumbo kwenye mkutano wa hadhara baada ya kukamilisha ziara ya kamati ya ulinzi na usalama ya kutatua migogoro ya ardhi.

Alisema katika kipindi hiki ambacho mvua imeanza kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini, kuna hatari ya magonjwa ya mlipuko kuanza kutokea endapo hawataweka mazingira yao katika hali ya usafi.

Aliwaagiza viongozi wa kata kutumia sheria ndogo za halmashauri kuwachukulia hatua watu wanaokiuka maagizo hayo kwa kuwa magonjwa hayo yakilipuka yanawaumiza hata wasiokuwa na hatia.

"Simamieni usafi kwenye maeneo yenu, zipo sheria ndogo za halmashauri zinazoeleza adhabu mbalimbali kwa watu wanaokiuka taratibu zetu, zitumieni kuwawajibisha wanaochafua mazingira," alisema.

Aliwaelekeza wananchi hao kujisimamia kuanzia kwenye ngazi ya kaya hadi kwenye eneo la biashara huku akiwataka watendaji wa kata na vijiji kuwapa siku saba kufanya usafi kwenye maoeneo yao.

Diwani wa Ifumbo, Weston Mpyila, aliahidi kushirikiana na viongozi wa serikali katika kata yake kuhamasisha usafi wa mazingira na shughuli mbalimbali za maendeleo ndani ya kata hiyo.

Alisema serikali imepeleka fedha nyingi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa miradi mbalimbali ya afya, barabara, elimu na maji.

Aliiomba serikali kuwasaidia kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya cha kata hiyo ambacho kilianza kujengwa tangu mwaka 2016 lakini mpaka sasa bado hakijakamilika kwa kukosa Sh. Milioni 77.

Ofisa Madini Mkazi Wilaya ya Chunya, Laurent Mayalla, aliahidi wananchi wa kata ya hiyo kuwa atakwenda kuwapa elimu ya madini na utunzaji wa mazingira. Alisema serikali inataka wananchi washiriki kwenye sekta hiyo wakiwa na elimu sahihi itakayowasaidia kuchimba kisasa na kujiinua kiuchumi.



## SMZ yajipanga kuendeleza maeneo ya viwanda

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema imejipanga kuyaendeleza maeneo ya viwanda ya Chamanangwe Pemba ikiwa ni juhudi na mikakati ya kukifungua kisiwa cha Pemba katika uwekezaji na kukuza uchumi.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha baraza la wawakilishi huko Chukwani nje ya mji wa Zanzibar na Waziri wa nchi ofisi ya rais kazi uchumi na uwekezaji Mudrik Ramadhan Soraga, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Viti maalumu, Shadya Mohamed Suleiman, aliyetaka kujua mikakati ya ujenzi wa viwanda katika eneo la Chamanangwe, Pemba umefikia hatua gani hadi sasa.

Soraga alisema, azma ya serikali ya awamu ya nane ni kukifungua kisiwa cha Pemba katika sekta ya uwekezaji hatua ambayo kwa kiasi kikubwa itasaidia kuzalisha ajira na kukuza uchumi wa wananchi.

Alisema jumla ya kampuni nne zimeonesha nia ya kuwekeza katika eneo la Chamanangwe, Pemba ikiwamo kampuni za kuzalisha umeme wa jua kwa mahitaji ya kisiwa hicho.

Aidha, alisema wawekezaji wamejitokeza kuwekeza viwanda vya kuchakata matunda na maombi ya uwekezaji yamepokewa.

Soraga alisema kazi kubwa inayofanywa kwa sasa ni kuweka miundombinu muhimu ikiwamo majisafi na salama pamoja na umeme.

Soraga alisema kazi ya ujenzi wa miundombinu mingine kwa ajili ya kukifungua kisiwa cha Pemba inaendelea ikiwemo ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba na maandalizi ya ujenzi yamekamilika kwa asilimia mia moja.

Aidha, alisema kazi ya ujenzi wa baadhi ya bandari za Pemba unaendelea hatua ambayo inakwenda sambamba na mikakati ya kukifungua kisiwa hicho na kukiunganisha na nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Kati.

"Hiyo ndiyo mikakati yetu kuona kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakwenda kukifungua kisiwa cha Pemba katika ujenzi wa viwanda pamoja na miundombinu hatua ambayo itakiunganisha kisiwa hicho na nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki," alisema.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, alisema serikali imetenga maeneo ya Dunga, Wilaya ya Kati Unguja pamoja na Pangatupu, Kaskazini Unguja kwa ajili ya ujenzi wa viwanda.

"Mheshimiwa Spika kwa upande wa Unguja tumetenga maeneo ya Dunga pamoja na Pangatupu kwa ajili ya ujenzi wa viwanda ambapo maeneo hayo tayari yamepimwa," alisema.

# ZFB yalalamika gharama upakuzi mizigo kupanda

**Na Mwandishi Wetu**

JUMUIYA ya Wakala wa Forodha Zanzibar (ZFB), wamesema gharama za upakuzi na usafirishaji wa mizigo zimepanda kwa kiwango kikubwa katika Bandari ya Malindi tangu serikali kubinafsisha shughuli za bandari kwa kampuni ya Zanzibar Multipurpos Terminal (ZMT) kutoka nchini Ufaransa.

Rais wa Jumuiya hiyo, Omar Hussein Mussa, alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari mjini Unguja, baada ya mawakala wa forodha kugoma kutoa mizigo wakipinga tozo zilizoongezeka katika shughuli zao.

"Tunakuwa na changamoto kidogo tangu Septemba 18 tulipowakabidhi hawa wawekezaji katika bandari yetu tulitaraji kwamba kwa mujibu wa mwenendo wa serikali na sisi wenyewe ni kuboresha huduma za bandari na kupunguza gharama za usafirishaji ambazo zipo juu sana ikilinganishwa na bandari zingine, sasa matarajio tuliyoyategemea kwa kweli hatujayapata na tumerudi nyuma kwa kiasi kikubwa, tunaamini jambo linaloendelea hivi sasa la Bandari ya Zanzibar sio dhamira ya serikali, rais, wananchi wakati dhamira ilikuwa njema za kupunguza gharama na bandari hii kufikika," alisema.

Alisema kwa bahati mbaya tangu kupatikana kwa mwekezaji huyo, kuna changamoto nyingi na hakuna mabadiliko yoyote yaliofanyika ya kuimarisha huduma katika bandari hiyo.

"Tunachokiona kwa upande wa mwekezaji ni kuhakikisha kwamba kile anachokitafuta sio kuwekeza bali ni kukusanya tu mapato na kuongeza tozo tofauti na matarajio ya wadau katika sketa ya usafiri, uchukuzi na usafirishaji," alisema.

Alitoa mfano wa kontena moja la mizigo la futi 20 limeongezewa tozo ya dola 400 wakati kontena la futi 40 limeongezewa tozo ya dola 800 huku shughuli za ukaguzi wa mizigo zikionekana kusuasua kutokana na kutengwa kwa eneo moja pekee la ukaguzi likiwa halina huduma zozote za usalama wa mizigo.

Alisema utoaji wa mizigo umepungua kwa kiwango kikubwa kutoka kontena 150 hadi 50 kwa siku huku meli nyingi za mizigo zikiamua kushusha mizigo ya Zanzibar katika Bandari ya Mombasa Kenya na Dar es Salaam na kusafirishwa kidogo kidogo Zanzibar.

Aidha alisema tozo za makontena katika Bandari ya Malindi, Unguja zimekuwa kubwa wakati Dar es Saalam kontena ya futi 20 ikitozwa dola 1,500 na dola 3000 kwa kontena la futi 40, lakini Zanzibar gharama zake ni mara mbili zaidi.

Wakala wa Forodha, Muhammed Said, alisema kuna mambo matatu yamejitokeza tangu wawekezaji hao walipokabidhiwa Bandari ya Malindi ikiwamo ucheleweshaji wa kutoa mizigo, utozajwi wa gharama za kuchelewa kutoa mizigo bila ya kuangalia chimbuko la tatizo na kusababisha kuwabebesha mzigo mkubwa wafanyabiashara.

"Wakati mwingine taratibu zote za utoaji wa mizigo unakua umezikamilisha, lakini wao ndio wanaochelewa kutoa makontena na unatozwa muda wa ucheleweshaji wa utoaji mizigo dola 20 mpaka 40 kwa siku hii sio haki," alilalamika.

Juma Issa Mussa wakala forodha, alisema wamiliki wa meli wamekuwa wazito kufika Zanzibar kutokana na gharama za meli kuegesha katika bandari kuongezeka tangu wawekezaji kukabiliwa uendeshaji wa Bandari ya Malindi Zanzibar.

"Zamani tozo za mzigo zilikuwa zikitozwa baada ya mzigo kushushwa, lakini sasa meli inapofunga gati tu gharama zinaanza kutozwa jambo ambalo linawapa gharama kubwa wasafirishaji wa mizigo na watu wanaoumia ni wananchi wa chini," alisema Juma.

Alisema mizigo haiko salama kutokana na kutengwa eneo moja tu la ukaguzi wa mizigo na kuwa katika hatari ya kuharibika hasa mvua inaponyesha na kusababisha ucheleweshaji wa kutoa mizigo usiokuwa na msingi.

Akizungumzia changamoto hizo, Waziri wa Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano, Dk. Khalis Mohamed Salum, alisema serikali imeamua kuunda kamati maalum na kuwashirikisha wadau katika sekta ya uchukuzi na usafirishaji kushughulikia changamoto zilizojitokeza katika bandari hiyo.

Mgogoro wa mawakala wa forodha Zanzibar na kampuni ya ZMT ulichukua sura mpya Novemba 28 baada ya mawakala kugoma kwa mda kutoa mizigo bandarini na kuahidi kuitisha mgomo kuazia Desemba 4, mwaka huu iwapo matatizo yaliojitokeza hayatopatiwa ufumbuzi na kampuni ya ZMT pamoja na serikali.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Richard Mchumvu akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana, kuhusu tukio la watuhumiwa wawili kulawitiana ndani ya chumba cha mahabusu ya Kituo cha Polisi Mwembe Madema mjini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mtuhumiwa ulawiti, ashtakiwa tena kulawitiwa mahabusu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MTUHUMIWA wa kosa la ulawiti amefunguliwa shtaka lingine baada ya kufanya tukio la kulawitiwa na mtuhumiwa mwezake wakiwa katika chumba cha mahabusu kituo cha Polisi Mwembe Madema, Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi wa mkoa huo Richard Mchumvu, alisema kosa la kwanza anatuhumiwa na wenzake 12 kuwa na mtandao wa masuala ya ulawiti na walikuwa chini ya uchunguzi wakati wakisubiri kupelekwa mahakamani.

Alisema mkasa wa tukio hilo ulitokea Novemba 22, mwaka huu, wakiwa wamehifadhiwa katika chumba cha mahabusu akifanyiwa kitendo hicho na mtuhumiwa mwenzake ambaye alifikishwa polisi kwa kosa la udhalilishaji la kumpiga mke wake wa ndoa.

"Mfanyaji wa ulawiti na mtuhumiwa mwenye umri wa miaka 40 ambaye alifikishwa kituoni hapa kwa kosa la kupiga mkewe na mtuhumiwa aliyelawitiwa ana umri wa miaka 22 alifikishwa kituoni hapa kwa kosa la ulawiti," alisema Kamanda huyo.

Aidha, alisema kwa kawaida watuhumiwa uhifadhiwa katika vyumba tofauti kati wenye umri mkubwa, watoto na wenye tatizo la afya ya akili.

Alisema askari polisi wakiwa katika ukaguzi katika mahabusu hiyo walipopokea taarifa ya mahabusu kulawitiana huku wenzao wakiwashuhudia.

"Ikiwa watu wanalawitiana ndani ya kituo cha polisi je hali ikoje kwa watoto huko katika jamii ambapo muda mwingi watoto wapo shuleni, madrasa au mitaani hivyo ni vyema jamii kuchukua tahadhari kubwa ya kuwalinda watoto hali ni mbaya mno," alisema.

Alisema kwa mwezi Novemba, mwaka huu wamefaniwa kuwakamata watuhumiwa 11 kwa makosa ya ulawiti na 10 kwa makosa ya ubakaji na jumla ya watuhumiwa 139 wa makosa mbalimballi ya kihalifu wamekamatwa. "Wahalifu waliohusika na wizi ni 84, kubaka 10, shambulio 27, njia ya udanganyifu wa kujipatia fedha watatu, ulawiti 11 na unyang'anyi mitaani, wanne," alisema.

Alisema Novemba 9, mwaka huu maeneo ya Bububu vijana watatu walikamatwa kwa kumbaka msichana mwenye umri wa miaka 17 ambao wanatuhumiwa kwa kosa la ubakaji wa kundi na upelelezi wa kesi huo unaendelea.

Alisema kuanzia Novemba mosi hadi 29 watu 18 wametiwa hatiani kwa makosa ya ubakaji, ulawiti, kuingilia kinyume na maumbile na shambulio," alisema. Aliitaka jamii kuacha kusuluhishana katika ngazi ya familia kwa matukio ya udhalilishaji na badala yake awe tayari kutoa ushahidi ili matukio hayo yachukuliwe hatua za kisheria.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ATUPELE ALLADIN**
anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 687 EBP - TOYOTA PICK – UP. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya Polisi:
**PHQ/DAR/KIN/47767/2023**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**FARIDA HAMISI KITEMWE** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba TAE 514311 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam November, 2022. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/MTW/MTW/1469/2023.**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**CHAMWINO MJINI DODOMA**
**Wilaya ya MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai/Ndoa Na 289/2023**
**Jina la mdai ALLEN CHIBARUA**
**Jina la mdaiwa EDGER EDSON**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo )**

**Kwa EDGER EDSON**

**Kwakuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa Habari za Madai ) TSHS 5,100,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 12 Mwezi 12 Mwaka 2023 saa 02:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 28 Mwezi 11 Mwaka 2023

..............................
**HAKIMU**

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**
**SHAURI NO. 64/2023**
**MUHIDHILI HARIDI LIKAMBA::::::::::MDAI**
**DHIDI YA**
**1.ANDY HARDSONY BUCKEY::::::::::MDAIWA**
**2.HADIJA IDDY ALLY:::::::::::::::::::::MDAIWA**
**3.RESTITUTA GODFREY::::::::::::::::MDAIWA**
**4.FRED PETER BARITE:::::::::::::::::::MDAIWA**
**YAH: KUITWA SHAURINI**
**KWA:FRED PETER BARITE**
**Fahamu kwamba MUHIDINI HARIDI LIKAMBA amefungua shauri dhidi yenu katika baraza hili.**

Shauri limepangwa kutaajwa tarehe 04/12/2023, saa 2:30 asubuhi mbele ya Mhe.T.Munzerere Mwenyekiti wa baraza.Mnatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Mnaamriwa kuhudhuria mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka:Msipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo nyie kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 27/11/2023.

**T.Munzerere**
**MWENYEKITI**
**27/11/2023**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOKO SONGEA**
**MAOMBI NAMBA 53/2023**

**JOSEPH LAURENT TOLLE......MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**ABDU NASSORO TOLLE}**
**ELVIS JOSEPH HULUKA}.....WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

Mjibu maombi wa pili anataarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yenu. Hivyo basi inatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako au wote kwa pamoja siku ya tarehe 28/12/2023 saa 2:30 asubuhi .Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati zako za utetezi.
Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili bila kujali uwepo wako.
Imetolewa leo na nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 30/11/2023.

..............................
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W).**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER JOHN NDAIGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 868 DUA aina ya Volkswages POLO, Chassis No. WVWZZZ6RZAU001923, Engine No. CGG202163CGG. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Taarifa ya Polisi:
**PHQ/DOD/DOD/10471/2023.**


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

USITISHWAJI MAPIGANO

# Israel, Hamas wakubali kuongeza muda

**TELAVIV,** Israel

JESHI la Israel (IDF) limesema makubaliano ya usitishwaji mapigano na kundi la Hamas yataendelea.

Katika taarifa iliyotolewa na jeshi hilo ilisema hatua hiyo inatokana na juhudi zinazofanywa na wapatanishi kwa ajili ya kuendeleza mchakato wa kuwaachilia mateka.

Hata hivyo, Hamas ilijibu taarifa hiyo kuwa imekubali kuendeleza makubaliano hayo na Israel kwa siku ya saba nyingine, shirika la habari la Reuters liliripoti.

Jeshi la Ulinzi la Israel halikusema urefushaji wa makubaliano hayo yatakuwa kwa muda gani.

**Hadi kufikia juzi usiku, mateka 97 wa Israel waliachiliwa huru, huku wafungwa 180 wa Kipalestina wakiachiliwa huru.**

Makubaliano ya kusitishwa kwa mapigano Ukanda wa Gaza yalirefushwa baada ya Hamas kuipa Israel orodha mpya ya wanawake na watoto waliotekwa nyara.

Gazeti la Israel Hayom lilinukuu Ofisi ya Waziri Mkuu ikieleza kupitia mtandao wa X kwamba baraza la mawaziri la vita la Israel limeamua kwa kauli moja usiku wa Jumatano mapigano yataanza mara moja ikiwa Hamas haitatoa orodha mpya.

Tangazo hilo la kurefusha makubaliano lilitolewa zikiwa zimesalia dakika chache kabla ya muda wake awali kuisha jana. Nchi ya Qatar ambayo inasimama kama mpatanishi mkuu ilithibitisha juzi kwamba mapatano hayo yataendelea kwa siku nyingine.

Qatar ilikuwa katika mazungumzo makali ya kutafuta namna ya kurefusha muda wa usitishaji mapigano na kuungwa mkono na mataifa ya Misri na Marekani.

Hadi kufikia juzi usiku, mateka 97 wa Israel waliachiliwa huru, huku wafungwa 180 wa Kipalestina wakiachiliwa huru.

Kutokana na kuimarika kwa hali ya Amani Ukanda wa Gaza, malori yaliyobeba misaada ya kibinadamu, vifaa vya matibabu na mafuta pia yameruhusiwa kuingia eneo hilo.

Katika hali isiyotarajiwa, Israel jana iliwaachilia huru Wapalestina wengine 30, kulingana na taarifa ya idara yake ya magereza.

Bado haijatolewa ufafanuzi kuhusu wafungwa hao kutokana na kutowekwa wazi majina, jinsia na umri wao.

Hapo awali, mateka wengine 10 wa Israeli na raia wanne wa Thailand waliachiliwa na Hamas.

Wakati huo huo, Umoja wa Mataifa umetoa wito wa kuundwa mataifa mawili katika kukomesha mzozo kati ya Israel na Hamas.

Umependekeza mji wa Jerusalem ambao umekuwa chanzo cha mvutano kutumika kama makao makuu ya mataifa hayo mawili.

Umoja huo pi umetoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kuendeleza jitihada za kupatikana suluhisho la uwepo wa mataifa mawili katika kukabili mzozo wa Wapalestina na Israel.

Akitoa hotuba iliyoandikwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Umoja wa Mataifa jijini Geneva Tatiana Valovaya, alisema sasa ni wakati wa kusonga mbele na dhamira ya wazi na sio kurudi nyuma.

Iliongeza kuwa hatua hiyo inaaanisha Israel na Palestina wanatakiwa kuishi kama majirani kwa amani na usalama huku Jerusalem ikitumika kama mji mkuu wa mataifa hayo mawili. **BBC**

# Bibi wa miaka 70 ajifungua mapacha

**KAMPALA,** Uganda

BIBI wa miaka 70 nchini Uganda amevunja rekodi na kuwa mwanamke wa kwanza barani Afrika mwenye umri mkubwa kujifungua watoto mapacha.

Kulingana na taarifa inaeleza mwanamke huyo alijifungua watoto mapacha baada ya kupata ujauzito kupitia matibabu ya kupandikiza (IVF).

Kituo cha Kimataifa cha Hospitali ya Wanawake na Kituo cha Uzazi ambacho kipo mji mkuu wa Kampala, kilisema Safina Namukwaya alijifungua mtoto wa kike na wa kiume.

"Hadithi hii haihusu tu mafanikio ya matibabu, inaonyesha nguvu na uthabiti wa roho ya mwanadamu," Hospitali hiyo ilisema katika mtandao wa Facebook.

Ilieleza bibi Namukwaya alijifungua kwa njia ya upasuaji kutokana na umri wake.

Aidha, Namukwaya alikiambia kituo cha TV cha NTV kwamba ilikuwa uzazi wake wa pili ndani ya miaka mitatu, baada ya mtoto wake wa kwanza wa kike kujifungua 2020. Alisema wakati akiwa mjamzito alipata matatizo mengi ikiwamo kutengwa na baba wa watoto hao.

"Wanaume hawapendi kuambiwa umebeba zaidi ya mtoto mmoja, tangu nilipolazwa hapa hajawahi kufika," alisema.

Hata hivyo Namukwaya alisema hajui atawezaje kuwalea watoto hao, lakini anafurahi kuwa nao baada ya miaka mingi ya kuvumilia unyanyapaa na kejeli kwa kukosa watoto. **BBC**



Bibi Safina Namukwaya akipongezwa na daktari baada ya kujifungua watoto mapacha katika hospitali maalum ya wanawake na uzazi nchini Uganda. **PICHA: WHIFC**

# Wasichana wachangamkia fursa masomo ya ubaharia

**Na Restuta James**

MKUU wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Dk. Tumaini Gurumo, amesema kuna ongezeko la wasichana kuchangamkia fani za bahari ukiwamo ubaharia, huku akiwataka wazazi na walezi kuwaruhusu mabinti kujiunga na chuo hicho chenye soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Aidha, serikali imeahidi kukipatia chuo hicho meli maalumu kwa ajili ya mafunzo ya vitendo, ili kuongeza ubora wa ujuzi unaotolewa chuoni hapo.

Akizungumza jana wakati wa mahafali ya 19 ya chuo hicho, Dk. Tumaini alisema wazazi wanapaswa kuondokana na fikra ya kudhani ubaharia ni fani ya wanaume pekee kwa kuwa wasichana nao wanafanya vizuri.

"Mwaka huu tumekuwa na wahitimu 1,326 na kati ya hao kuna ongezeko kubwa la wanafunzi wa kike kutoka 209 mwaka jana hadi 403, hii kwetu ni dalili njema… ninatoa rai kwa wazazi na walezi wawaruhusu vijana wao wa kike na wa kiume kusoma fani mbalimbali za bahari zinazotolewa hapa," alisema.

Alisema sekta ya bahari inaendelea kukua kutokana na uwekezaji unaoendelea kufanywa na serikali hususani ujenzi wa meli na mpango wa kujenga kiwanda cha kuunda meli nchini.

Akizungumza kabla ya kutunuku vyeti kwa wahitimu, Naibu Waziri wa Wizara ya Uchukuzi, David Kihenzile, alisema serikali itahakikisha inatatua changamoto ya ukosefu wa meli ya mafunzo katika chuo hicho ili kuboresha taaluma kwa wanafunzi.

# Wanahabari watakiwa kuelimisha falsafa ya 'R 4'

**Na Beatrice Moses**

WANAHABARI wametakiwa kuielimisha jamii umuhimu wa kutekeleza falsafa ya Rais Samia Suluhu Hassan ya 'R' nne katika kuleta mabadiliko ya kiutendaji nchini.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, alisema hayo wakati akiwasilisha mada kwenye Maadhimisho ya miaka 36 ya Chama cha Wanahabari Wanawake Nchini (TAMWA) yaliyoanza jana jijini Dar es Salaam.

Matinyi alisema falsafa hiyo ikitekelezwa kwa vitendo itasaidia kuleta maendeleo na kujenga upya nchi.

Alisema viongozi wa nchi wanapokuwa madarakani hutumia falsafa zinazowasaidia kuongoza kuleta mbadiliko katika uongozi wao. Akitoa mfano wa Rais wa kwanza Hayati Mwalimu Julius Nyerere ya Uhuru na Kazi.

Akiifafanua falsafa hiyo ya 4R, alisema ni Maridhiano, (Reconciliation), Mageuzi (Reform), Ustahimilivu (Resilience) na Kujenga upya (Rebuilding) ni falsafa anayotumia Rais Samia katika uongozi wake.

"Mfano hapo awali kulikuwa na zuio kwa vyama vya upinzani kufanya mikutano, serikali chini ya Rais Samia imeruhusu, pia kuna Tume ya haki jinai imefanya kazi kubwa wananchi wanapaswa kujulishwa," alisema.

Mwenyekiti wa TAMWA, Joyce Shebe, katika hotuba yake alisema kuwa tunafurahishwa na mafanikio yaliyopatikana hata hivyo bado kuna changamoto zinazo changiwa na umaskini.

"Tafiti zinaonesha kwenye vyumba vyetu na vyumba vya habari bado kuna changamoto ya rushwa ya ngono hali inayoshusha weledi wa tasnia."

Naibu Waziri wa Habari na Mawasiliano, Kundo Mathew, akimwakilisha Waziri wa Habari, Nape Nnauye, alisema ni furaha kuona mafanikio ya TAMWA.

"Kutokana na Maendeleo ya sanyansi na teknolojia ni nia yetu kuona wanawake wanapata mafunzo ya sayansi na teknolojia ili kukuza uwezo na uelewa wao," alisema Shebe.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben amesema ilipofika Julai mpaka Septemba kupitia sapoti ya wadau wetu, tukafanya utafiti ya hali ya unyanyasaji wa kijinsia katika vyombo vya habari.

Alisema kuna unyanyasaji wa kingono ambao, wanaukemea kwa kuwa wanaamini unapunguza weledi kwa waandishi.

"Utafiti huu ulihusisha vyombo 17 na wanahabari 137 Tanzania na Zanzibar. Ripoti ya utafiti huo iliyozinduliwa juzi, ilionesha asilimia 59 waliripoti kuwa wanapitia unyanyasaji huo ndani ya vyombo vyao vya habari," alisema.

Alisema kuwa utafiti huo uligundua kuna aina ya kawaida ya unyanyasaji wa kijinsia na wahusika wakuu wa unyanyasaji wa kingono ni wenye madaraka makubwa ndani ya vyombo vya habari," alisema Dk. Rose.

Mkurugenzi wa Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari nchini (UTPC), Kenethy Simbaya, alisema wanatambua masuala ya usalama kwa wasichana katika kukuza ujuzi wao katika vyombo vya habari, ikiwamo ukatili wa kijinsia hususani, rushwa ya ngono.

# KMC YAPIGA HESABU KALI IKIWAALIKA MASHUJAA FC

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa KMC FC , Abdihamid Moallin, amesema kikosi chake kiko kamili na tayari kuondoka na alama tatu muhimu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mashuja FC utakaochezwa keshokutwa.

**KMC FC itawakaribisha Mashujaa kutoka mkoani Kigoma kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam kuanzia saa 10:00 jioni.**

KMC FC ikifanikiwa kushinda mchezo huo itafikisha pointi 19 sawa na Simba ambao wako nafasi ya tatu lakini itawashusha Singida Fountain Gate yenye pointi 18.

Akizungumza na Nipashe jana, Moalini alisema baada ya kutoka sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya Kagera Sugar, wamerejea kwenye uwanja wa mazoezi na kufanyia kazi mapungufu mbalimbali ili kuivaa Mashujaa wakiwa imara zaidi.

Moallin alisema kazi yake kubwa anayoifanya ni kuimarisha safu ya ulinzi na ushambuliaji ili kutofanya makosa yaliyojitokeza katika mechi iliyopita na hatimaye kufikia malengo.

"Tunaendelea na maandalizi ya kufanyia kazi mapungufu yetu kabla ya kufikiria dirisha dogo la usajili tutafanya nini, kwa sasa tunasahihisha makosa yetu, akili na nguvu zetu tunahitaji alama tatu dhidi ya Mashujaa FC.

Suala la usajili litafanyika muda ukifika na tutaangalia zaidi safu ya ulinzi na ushambuliaji ambayo ina changamoto na inahitaji marekebisho makubwa. Siwezi kusema kama tutaongeza mchezaji ila mpaka kufika nusu msimu malengo yangu ni kusalia katika nafasi tano au sita za juu," alisema kocha huyo.

Aliongeza anawapongeza wachezaji wake kwa kuendelea kupambana kusaka pointi katika kila mechi wanayocheza na msimu huu anahitaji kufika mbali kwenye michuano ya Kombe la FA.

"Kuwa chini ya vigogo kama Simba, Yanga na Azam sio jambo rahisi, ninawapongeza wachezaji wangu ingawa makosa yapo ila muda wa kuyarekebisha ni mkubwa na hakuna kitakachoharibika," aliongeza Moallin.



Wachezaji wa KMC FC wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mashujaa itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## *Mafunzo yaipunguza kasi KVZ*

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

MAAFANDE wa Mafunzo wameibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya KVZ FC katika mechi ya mzunguko wa 13 wa Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa Visiwani hapa juzi.

Ushindi huo ni watatu mfululizo na umeifanya Mafunzo ifikishe pointi 14 na kupaa hadi katika nafasi ya 10 huku KVZ FC yenye pointi 23 ikisalia katika nafasi ya tatu.

Akizungumza Kwa furaha baada ya mechi kumalizika, Kocha Mkuu wa Mafunzo, Abdallah Bakari "Edo" alisema wamepata ushindi mnono katika kipindi ambacho timu yake ilikuwa inahitaji sana pointi ili kujiondoa katika mstari wa hatari.

Edo alisema ushindi huo umetokana na jitihada zilizoonyeshwa na wachezaji ambao walikuwa na ari ya kuvuna alama tatu baada ya kupata matokeo mabaya mapema mwanzo wa msimu.

"Ushindi wa leo (juzi), umetusaidia kujiondoa katika mstari mwekundu kama lengo letu lilivyokuwa hapo awali. Tumecheza na timu bora, timu ambayo ipo katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu na tumevuna pointi tatu, tumeshinda kipindi ambacho tunahitaji tushinde michezo iliyobaki ili tutoke katika mstari mwekundu katika mzunguko huu," alisema Edo.

Aliongeza baada ya kumaliza mechi hiyo kwa mafanikio, sasa wanaelekeza macho na akili kuelekea mchezo unaofuata wa raundi ya 14 dhidi ya Uhamiaji FC utakaofanyika Desemba 9, mwaka huu.

Alisisitiza pia katika mechi hiyo wanahitaji kupata ushindi na anaamini maandalizi mazuri wanayofanya yatazaa matunda ingawa wanafahamu mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu wapinzani wao wamepoteza mechi iliyotangulia.

## Kisiwani mabingwa Upendo Super Cup

Na Mwandishi Wetu

VIJANA wametakiwa kujihusisha na michezo mbalimbali kwa lengo la kuupa mwili mazoezi na kutojihusisha na makundi ya kihalifu pamoja na matumizi ya dawa za kulevya, Mkurugenzi Mtendaji wa gazeti la Tanzania Leo, Frank Malaki, alisema wakati wa kufunga mashindano ya Upendo Super Cup.

Malaki aliwataka vijana kuzidi kujikita zaidi kwenye mazoezi ili kuimarisha mwili, umoja na mshikamano katika kristo kwa kudumisha upendo na amani.

Timu ya KKKT ya Mtaa wa Kisiwani ilitwaa Kombe la Upendo Super Cup baada ya kuwafunga Tabata Shule kwa changamoto ya penalti 8-7, baada ya kufungana bao 1-1 katika muda wa kawaida.

Nafasi ya tatu katika mashindano hayo ilichukuliwa na Boko Ushirika baada ya kuwafunga waandaaji wa mashindano hayo Mabibo External penatli 6-5 na kuzawadiwa seti ya jezi na mpira.

Edwin Mbiza, mshambuliaji wa Mabibo External aliibuka mfungaji bora wa michuano hiyo akipachika mabao matano, huku kipa wa mabingwa, Robert Masala, akitangazwa golikipa bora.

## Timu 21 zachuana Wakili CUP

Na Shaban Njia, KAHAMA

TIMU 21 zinachuana kuwania ubingwa wa mashindano ya Ligi Daraja la Nne (Wakili Nkuba KDFA 2023) yanayofanyika kwenye Uwanja wa Taifa wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani, Shinyanga imefahamika.

Bingwa wa mashindano atapata zawadi ya Sh. milioni tano, mshindi wa pili atapewa Sh. milioni tatu na timu itakayomaliza katika nafasi ya tatu itakabidhiwa Sh. milioni moja.

Mratibu wa Mashindano, Conrad Nkuba, alisema michuano hiyo inafanyika kwa kushirikiana na Chama cha Soka Wilaya ya Kahama (KDFA) pamoja na cha mkoa wa Shinyanga (SHIREFA).

Nkuba alisema jumla ya Sh. milioni 40 zitatumika kuendesha mashindano hayo ya mwaka huu ambapo kutakuwa na zawadi ya mchezaji bora, kipa bora, kiungo bora na mfungaji bora.

Mwenyekiti wa KDFA, Salum Hussein, alisema msimu wanafuraha kupata mdhamini kwa mwaka huu na anaahidi mshindi atapatikana kwa kufuata kanuni 17 za mchezo huo na kuongeza michuano hiyo itamalizika Desemba 7, mwaka huu.

## ZISIKUPITE

### SALAH SASA KUUZWA

KUUZWA kwa fowadi wa Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 31 msimu ujao kunaweza kufungua milango kwa Liverpool kumsajili nyota wa Ufaransa, Kylian Mbappe (24). ***(Team Talk)***

### MARTINEZ MAMBO SAFI

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lautaro Martinez, anatarajiwa kusaini mkataba mpya na Inter Milan, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kuhusishwa na Chelsea na Manchester United. ***(90 Min)***

### DENDONCKER KUTUA EVERTON

EVERTON inamfuatilia kiungo wa kati wa Aston Villa, Leander Dendoncker, wakati dirisha la uhamisho la Januari likikaribia, huku klabu hiyo ya Midlands ikiwa tayari kusikiliza ofa kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 28. ***(Football Insider)***

### EVERTON, CRYSTAL VITANI

EVERTON pamoja na Crystal Palace, pia wanavutiwa na kiungo wa kati wa Leicester City na Timu ya Taifa ya Ireland, Kasey McAteer, mwenye umri wa miaka 22. ***(Football Transfers)***

### SPURS: HOJBJERG HAONDOKI

KLABU ya Tottenham Hotspur huenda ikalazimika kukataa ofa kwa kiungo wa Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye umri wa miaka 28 na kiungo wa kati wa England, Oliver Skipp (23), huku mchezaji wa kimataifa wa Uruguay, Rodrigo Bentancur (26), akiwa nje hadi Februari mwakani kutokana na jeraha la kifundo cha mguu alilopata. ***(Telegraph)***

### KIWIOR ATAJWA MILAN

KLABU ya AC Milan itajaribu kupunguza matatizo yao ya safu ya ulinzi kwa kusaka kwa mkopo saini ya beki wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Poland, Jakub Kiwior, mwenye umri wa miaka 23 ifikapo Januari. ***(Calciomercato)***

### SANTOS KUREJEA CHELSEA

CHELSEA iko tayari kumrejesha kiungo wa kati wa Brazil, Andrey Santos, ifikapo Januari, kwa sababu klabu hiyo haijafurahishwa na hali ya sasa ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 akiwa kwa mkopo Nottingham Forest.***(Fabrizio Romano via kupitia X)***

### SAMED KUMRITHI LUIZ

KLABU ya Aston Villa imemtambua kiungo wa kati wa Lens na Ghana, Salis Abdul Samed, mwenye umri wa miaka 23 kama mbadala wa kiungo wa kati wa Brazil, Douglas Luiz (25), iwapo watalazimishwa kumuuza. ***(Team Talk)***

### GUIRASSY ANUKIA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inavutiwa na mshambuliaji wa Stuttgart na Guinea, Serhou Guirassy mwenye umri wa miaka 27 ili kuimarisha safu yao ya ushambuliaji. ***(Rudy Galetti kupitia X)***

### COOPER, MABOSI SAFI

KOCHA wa Nottingham Forest, Steve Cooper, anaungwa mkono kikamilifu na mmiliki wa klabu hiyo, Evangelos Marinakis, ingawa Mgiriki huyo anataka kuona kuboreshwa kwa matokeo ya timu yake. ***(Telegraph)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# TEN HAG: NILAUMIWE MIMI KUTOLEWA UTD

**ISTANBUL,** Uturuki

### ●●● Kocha huyo ajitetea timu iko katika maboresho na lakini...

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, amesisitiza lawama za mwisho kwa timu yake kutolewa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ziko mlangoni pake, lakini bado alikiri wachezaji pia wanastahili kukosolewa.

**United waliingia kwenye mchezo dhidi ya Galatasaray uliochezwa juzi usiku wakitakiwa kupata ushindi baada ya kupoteza michezo mitatu kati ya minne ya mwanzo katika hatua ya makundi.**

Mambo yalianza vyema walipokuwa mbele kwa mabao 2-0, lakini Galatasaray ilitoka nyuma na kupata sare ya 3-3, licha ya Scott McTominay kuweka United mbele kwa 3-1.

"Ninawajibika kwa hili," alisema Ten Hag akiiambia TNT Sports.

"Tunajua tuko kwenye mradi, tunafanya maboresho, kwa hiyo nina matumaini makubwa. Tunaenda katika mwelekeo sahihi kwa hiyo najua tutafanikiwa kwa muda mrefu, lakini ukitaka kubaki Ligi ya Mabingwa Ulaya lazima ushinde michezo hii.

"Tulikuwa tunashinda halafu tunapoteza, tulipaswa kuchukua pointi tatu, hiyo ni wazi, tulifanya hivyo kwenye michezo mingine, nilifurahishwa na jinsi tulivyocheza lakini wakati huo huo lazima niikosoe timu kwa sababu ulinzi haukutosha.

"Tunaongoza 3-1 na hatuwezi kumudu makosa kwani inaleta madhara."

Nahodha wa United, Bruno Fernandes, pia akizungumza na TNT Sports, alikiri mabao waliyofungwa yalikuwa "mabaya sana" kutoka kwa mtazamo wa timu yake.

"Tulikuwa juu ya mchezo mara mbili na tulikuwa na nafasi nyingi sana za kufunga. Hatukuwa na umaliziaji mzuri," alisema Fernandes.

"Sitaki kuwa hasi sana, lakini kile ambacho tumekuwa tukifanya kwenye Ligi ya Mabingwa hakitoshi, sio mchezo wa kwanza kuwa hivi, lazima tupate matokeo, lazima tuelewe aina hizi za michezo na hatua tunazopaswa kuchukua.

"Kila mtu anapaswa kuchukua hatua na kuwajibika kwa makosa yake mwenyewe."

# ANCELOTTI AFURAHISHWA NA UBORA WA BELLINGHAM




**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti alimlinganisha, Jude Bellingham na Zinedine Zidane baada ya kiungo huyo kuibuka mchezaji bora wa mechi katika ushindi wa mabao 4-2 ambao Real Madrid imeupata dhidi ya Napoli kwenye mechi ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi usiku.

Bao la kichwa la Bellingham liliifanya Madrid kuwa mbele kwa mabao 2-1 katika mchezo wa Kundi C kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu, baada ya Giovanni Simeone kuiweka Napoli mbele na Rodrygo kuwasawazishia wenyeji.

Frank Zambo Anguissa wa Napoli alifanya matokeo kuwa 2-2 baada ya muda wa mapumziko na chipukizi Nico Paz akarejesha uongozi wa Madrid, kabla ya Bellingham kutoa pasi ya goli kwa Joselu na kupata ushindi katika muda wa nyongeza.

"Ni vigumu kulinganisha vizazi viwili tofauti," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi alipoulizwa kuhusu kulinganishwa na Zidane, ambaye alikuwa jukwaani akitazama mchezo huo.

"Ninachokiona ni uwezo wa Bellingham wa kuingia kwenye eneo la hatari. Zidane hakuwa na hilo. Na ubora wa mtu binafsi aliokuwa nao Zidane, Bellingham hana.

"Lakini hilo ni soka la kisasa. Soka la kisasa linahitaji wachezaji wa kimwili kama Bellingham, ambao wanaweza kucheza uwanja mwingi kwa haraka."

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England kwa sasa amefunga mabao 15 katika mechi 16 alizoichezea Real Madrid.

"Ilionekana kama alikuwa amechoka sana katikati ya kipindi cha pili," aliongeza Ancelotti.

# Martinez kubakia Inter Milan

**MILAN,** Italia

LAUTARO Martinez yuko tayari kusaini mkataba mpya na Inter Milan licha ya kutakiwa na Chelsea na Manchester United, kwa mujibu wa 90min.

Mkataba wa sasa wa nahodha huyo wa Inter, klabu hiyo ya San Siro unatarajiwa kumalizika ifikapo 2026, na wawakilishi wake wamefanya mazungumzo na Chelsea na United katika miezi 18 iliyopita kabla ya uwezekano wa kuhama kutoka Italia kwenda England.

90mi iliripoti Juni, mwaka huu klabu mbili za Ligi Kuu England pamoja na Real Madrid, zote zilionyesha nia ya kumsajili fowadi huyo wa Argentina.

Licha ya hayo, Inter waliendelea kumshikilia nyota wao wakati wa dirisha la usajili, na tangu wakati huo wamekuwa na nia kubwa ya 'kumfunga' mshambuliaji huyo kwa mkataba wa muda mrefu katika klabu hiyo, kabla ya majira ya joto ya 2024.

90min inaelewa Martinez sasa yuko tayari kusaini nyongeza ya mkataba na Nerazzurri hao baada ya kuwa na mwanzo bora kwa msimu wa 2023/24.

Nyota huyo raia wa Argentina amekuwa katika kiwango cha hali ya juu kwa Inter hadi sasa msimu huu, akifunga mabao 13 katika mechi 13 za Serie A - likiwamo bao muhimu la kusawazisha katika mchezo wa Jumapili wa dabi ya Italia dhidi ya wapinzani wao wakuu, Juventus kwenye Uwanja wa Allianz.

Kiwango cha nahodha huyo kimeifanya Inter kukaa kileleni mwa msimamo wa Serie A, pointi mbili mbele ya wapinzani wao wa karibu Juve, na pia kushinda mara tatu na sare katika mechi zao nne za kwanza za makundi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.



# Arteta: Ni zaidi ya ndoto zangu



**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, aliisifu timu yake baada ya kutinga katika hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa kwa kuifunga Lens mabao 6-0 usiku wa baridi kali kaskazini mwa London hapo juzi.

Ushindi wa Washikabunduki hao ulikuwa ni mkubwa zaidi kuupata kwa timu ya England dhidi ya wapinzani wa Ufaransa katika mashindano ya Ulaya.

"Sikuwa na ndoto kama hii," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari.

"Tulikuwa na nafasi ya kufuzu leo (juzi) na kuwa vinara wa kundi na nadhani tumefanya hivyo kwa njia ya kuridhisha.

"Timu tangu mwanzo ilionyesha kiwango na dhamira ya kushinda mchezo. Kila kitu kilifanyika kwa njia sahihi katika dakika 30 za kwanza."

Arteta alisema timu yake imekuwa ikionyesha hali kama hiyo nyumbani kwa muda, na anakaribisha ukweli wachezaji sita tofauti walikuwa na majina yao kwenye karatasi ya matokeo.

"Uthabiti ambao tumeonesha nyumbani kwa kutoruhusu bao lolote na kufunga ni jambo chanya," alisema.

Alikuwa na nia ya kupunguza matarajio yake katika mashindano makubwa ya vilabu barani Ulaya, hata hivyo.

"Sasa tusubiri. Tutajua Februari tunakabiliana na nani katika raundi inayofuata na tuone jinsi tulivyo katika wakati huo."

# DODOMA JIJI FC YALIA PENALTI YA PRISONS, KOCHA AFUNGUKA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupokea kipigo cha bao 1-0 juzi kutoka kwa Tanzania Prisons, Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji, Kassim Liogope amesema wamekubali matokeo, lakini ameilalamikia penalti waliyopata wapinzani wao haikuwa halali.

Akizungumza mara baada ya kumalizika mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Sokoine Mbeya, Liogope alisema mechi ilikuwa nzuri na timu zote zilicheza kwa kushambuliana kwa zamu na mbinu za hali ya juu, lakini kwa bahati mbaya wamepoteza mechi ambayo hawakupaswa kufanya hivyo, akisema wapinzani wao walipata penalti nyepesi mno.

**"Mechi ilikuwa na ushindani, wenzetu Prisons ni wazuri sana kwenye mipira mirefu, tulifanikiwa kuzuia njia zao za pembeni, hiki kilichotokea hatukutarajia kama kitatokea, wenzetu wamepata penalti ambayo kwangu naona ni nyepesi tu," alisema.**

Penalti hiyo ndiyo iliyozaa bao pekee kwenye mchezo huo, likiwekwa wavuni na Jumanne Al-Fadhil dakika ya 77 ya mchezo huo na kudumu kwa dakika zote 90.

Naye kocha mpya wa Tanzania Prisons, Ahmad Ally alisema mazoezi ya siku tatu tu aliyowapa wachezaji wake




wameanza kuleta mabadiliko chanya.

"Niwapongeze vijana kwa jinsi walivyofanya, hasa kuifunga timu ambayo ilikuwa na mfululizo wa matokeo mazuri, kwa siku tatu tu nilizofundisha wameweza kunielewa kwa jinsi nilivyotaka wacheze, nawapongeza sana na kama tutakwenda kwa mwenendo huu basi tutafanya vizuri mbele ya safari," alisema kocha huyo aliyechukua nafasi ya Fred Felix 'Minziro'.

Tanzania Prisons juzi ilishinda mechi yake ya kwanza tangu Oktoba 8 ilipoifunga Mtibwa Sugar mabao 3-2 kwenye uwanja huo.

Baada ya hapo ilicheza mechi tano bila kupata ushindi wowote, ikipoteza mechi mbili na kutoa sare michezo mitatu.

Kwa ushindi huo wa juzi sasa imepanda mpaka nafasi ya 13 kwenye msimamo ikikusanya pointi 10 baada ya kucheza mechi 11, Dodoma jiji yenyewe inabaki katika nafasi ya sita ikiwa na pointi 15 baada nayo kucheza michezo 11.



Vijana wakicheza mpira wa Kikapu kama walivyokutwa na mpiga picha kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Twiga Stars yanusa fainali za WAFCON

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya soka ya wanawake (Twiga Stars) wametanguliza mguu mmoja kushiriki fainali za Afrika (WAFCON) mwakani nchini Morocco baada ya jana kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Togo kwenye uwanja wa Azam Complex.

Mchezo huo ni wa kwanza kwa timu hizo kuelekea kwenye fainali hizo na sasa Twiga Stars inahitaji sare tu kwenye mchezo wa marudiano utakaochezwa Togo ili kujihakikishia kushiriki fainali hizo za mwakani.

Mwiba mchungu kwa timu ya Togo alikuwa mshambuliaji na nahodha wa Twiga Stars, Oppa Clement aliyeifungia Stars mabao mawili katika ushindi huo muhimu.

Oppa alianza kuiandikia Twiga Stars bao la kwanza katika dakika ya 44 kwa mkwaju wa penalti baada ya beki wa Togo kuushika mpira ndani ya eneo la hatari.

Goli la pili lilifungwa dakika 51 baada ya ya wachezaji wa Togo kujifunga wakiwa katika harakati za kuokoa mpira mrefu uliopigwa na beki wa Twiga Stars kumtafuta Oppa, lakini golikipa wa Togo akiwa kwenye harakati za kuokoa aliupiga mpira uliomgonga beki wake na kuelekea nyavuni.

Zikiwa zimesalia dakika tisa mpira kumalizika, Oppa aliwainua tena mashabiki kwa kufunga bao la tatu kwa shuti baada ya kupokea pasi kutoka kwa Stumai Abdallah aliyeingia kipindi cha pili.

Kwa matokeo hayo, Twiga Stars watakuwa na kazi ya kwenda kulinda ushindi wao ugenini na kama watafanikiwa watakuwa wamefuzu kushiriki fainali hizo za mwakani kwa mara ya pili.

Togo wenyewe ili waweze kuiondoa Twiga Stars na kufuzu kwa fainali hizo, watalazimika kushinda si chini ya mabao 4-0 katika mchezo wa marudiano utakaochezwa Desemba 5.

Ushindi huo pia unawapa uhakika Twiga Stars wa kupata shiilingi milioni 15 kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan aliyoahidi kutoa milioni 5 kwa kila goli litakalofungwa.

Mara ya mwisho Twiga Stars kuchezea fainali hizo za WAFCON ilikuwa mwaka 2010 wakiwa chini ya kocha Boniface Mkwasa, fainali hizo zilifanyika Afrika Kusini.

## *Jwaneng, Wydad kuamua hatima wakukatwa Simba*

INATOKA UKURASA 24

kama wanavyokusudia.

Alisema iwapo watashinda mechi hiyo, basi watakuwa na uhakika wa kuzipata pointi wanazozisaka kwa ajili ya kutimiza lengo lao namba moja msimu huu, kutinga hatua ya robo fainali, Ligi ya Mabingwa Afrika.




"Ni mchezo mgumu na muhimu kweli kweli kwetu, kwa sababu ndiyo mwanzo wa kuzitafuta pointi tisa za nyumbani.

Kwenye michuano hii kama huwezi kuzipata pointi za nyumbani, basi utakuwa kwenye wakati mgumu sana, utalazimika kufanya kila njia, ushinde mechi moja ugenini au utoke sare na kusikilizia matokeo ya mechi zingine kitu ambacho si rahisi sana kwenye soka la Afrika," alisema Kamwe.

Yanga itacheza mechi hiyo dhidi ya Mabingwa Watetezi, saa 1:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki.

## Jwaneng mikononi mwa Benchikha

INATOKA UKURASA 24

wachezaji majukumu yao, na nimewataka kuhakikisha wanajituma ili kuwapa furaha mashabiki, ninawaamini na kwa pamoja tunaweza kubadili hali ya hewa iliyopo sasa na kurudisha furaha kwa mashabiki, wanachama na wapenzi wa Simba kwa kuanza kupata ushindi Jumamosi," alisema Benchikha na kuongeza,

"Ni kweli kuna mechi muhimu mbele yetu, kazi tumeanza kuifanya, wachezaji wanaelewa nini wafanye, ki ukweli tunahitaji kushinda hiyo mechi, kila mmoja anatakiwa kujituma kwa ajili ya timu na kutumikia nembo ya klabu," alisema kocha huyo.

Aidha, alisisitiza kuwa anahitaji mchezaji ambaye anajituma na kufanya majukumu yake na hatakuwa tayari kumvumilia mchezaji yoyote ambaye atakwamisha utekelezaji wa majukumu na kufikia malengo yake.

Benchikha alisema anatambua ugumu michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika lakini anaimani wachezaji wakiamua kujitoa na kupambania klabu watafanikiwa katika malengo yao ya kutwaa mataji na kuvuka hatua ya robo na kwenda kucheza nusu fainali ya ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba watacheza mchezo wa kesho wakiwa na kumbukumbu ya kuondolewa na Wabotswana hao kwenye raundi ya kwanza baada ya kushinda ugenini mabao 2-0 mwaka 2021 lakini waliruhusu kipigo cha mabao 3-1 kwenye mchezo wa marudiano Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Michezo

Ijumaa Desemba 1, 2023

Nipashe



Twiga yanusa fainali za WAFCON UKURASA 23



Mshambuliaji wa Twiga Stars, Oppa Clement (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa Togo, Ayawoh Kaglan katika mechi ya raundi ya tatu ya kusaka tiketi ya kucheza Fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wanawake (WAFCON 2024), iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana, Twiga Stars ilishinda mabao 3-0. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# Gamondi amaliza kazi, kuanza kusaka pointi 9 nyumbani

●●● Kuwakabili Al Ahly kesho akiwa amefanyia kazi makosa yaliyowaponza kwenye mchezo uliopita, aahidi...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema kuwa pamoja na kupoteza mchezo wao wa kwanza hatua ya makundi wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CR Belouizdad, bado ana matumaini ya kusonga mbele na anataka kuhakikisha wanavuna pointi tisa kwenye michezo yao yote ya nyumbani.

**Miguel alisema wataanza kampeni hiyo kwenye mchezo wao wa kesho dhidi ya Al Ahly ambapo maandalizi kwa upande wake yamekamilika na wanausubiri tu mchezo huo muhimu kurejesha matumaini yao ya kutinga hatua ya robo fainali.**

Alisema amefanyia kazi mapungufu aliyoyaona kwenye mchezo wao wa kwanza walioucheza ugenini dhidi ya CR Belouizdad na kukumbana na kipigo cha mabao 3-0 ambapo Gamondi alirudia kusema kutowaheshimu wapinzani wao na kucheza bila nidhamu ndio sababu ya kipigo hicho.

"Nilisema, nidhamu kwenye mchezo ni kitu muhimu na hasa unapocheza na timu kubwa na bora hapa Afrika, katika mechi iliyopita tumefungwa mabao 3-0 kilichotugharimu ni nidhamu ya mchezo, makosa machache tu tuliyoyafanya tuliadhibiwa, unawaza usiadhibiwe na timu za kawaida tu, lakini siyo CR Belouizdad na Al Ahly, kwa hiyo nimekaa na wachezaji wangu kuelekezana jinsi gani ya kucheza na timu kama hizo pamoja na kuwa makini muda wote wa mchezo, lakini pia kuepuka makosa madogo madogo," alisema Gamondi ambaye ni kocha wa kwanza kupeleka timu hiyo hatua makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya miaka 25.

Hata hivyo kocha huyo hakutaka kuingia kwa undani sana akisema vitu vingine ni 'Siri ya kambi' kwani kama akivitoa anaweza kuwarahisishia kazi wapinzani wake wa kesho nao wakaamua kuja na mfumo mwingine.

Gamondi, alisema amefuatilia wapinzani wao wa kesho na tayari amewapa mbinu na maelekezo wachezaji wake na kazi imebakia kwao (wachezaji) kuwafurahisha mashabiki wao kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa.

Wakati kocha huyo akiyasema hayo, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe amesema mechi ya kesho ni muhimu sana kwao kwa sababu itawapa mwelekeo wa kuzipata pointi tisa za nyumbani

INAENDELEA UKURASA 23

# Jwaneng Galax mikononi mwa Abelhak Benchikha

**Na Saada Akida**

KOCHA mpya wa Simba, Abelhak Benchikha tayari amekabidhiwa faili la wapinzani wao Jwaneng Galaxy na ameahidi kuanza kurudisha furaha ya mashabiki wa timu hiyo kesho.

Simba, kesho itakabiliana na Jwaneng Galaxy ugenini saa 10:00 jioni kwenye mchezo wake wa pili hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kikosi cha Simba kinatarajia kuondoka nchini leo kuelekea Botswana kwa ndege ya kukodi tayari kwa ajili ya mchezo huo ambapo wameweka wazi hawataki kufanya makosa yoyote yatakayowanyima ushindi.

Akizungumza na Nipashe jana, Benchikha, alisema kazi kubwa inaanza kwake ni kufanyia kazi mechi iliyopo mbele yao kwa kusahihisha makosa yao katika mchezo uliopita lakini pia kufanyia kazi ubora wa wapinzani wao ambao wamewaona katika michezo yao iliyopita.

Alisema amekutana na kufanya mazungumzo na makocha aliowakuta kwenye timu hiyo kumfahamisha walipoanzia na walipofikia na kukabidhiwa masuala yote na Kocha huyo kuendelea walipoishia kwa kuanza kwenda kusaka matokeo chanya ugenini.

"Nimewakumbusha

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >